



**MAMLAKA YA MAWASILIANO  
TANZANIA**

# **Ripoti ya Hali ya Sekta ya Mawasiliano**

**Robo mwaka inayoishia Machi 2026**

**[www.tcra.go.tz](http://www.tcra.go.tz)**

**VIWANGO VYA ISO 9001:2015**

# Muhtasari

Sekta ya mawasiliano imeendelea kukua na kuthibitisha mchango wake katika kuendeleza mageuzi ya kidijitali na maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini Tanzania. Sekta hii imeendelea kuwa himilivu na yenye kuendana na mabadiliko, ikichochoewa na ongezeko la uwekezaji na watumiaji wa huduma za mawasiliano ya simu, intaneti, utangazaji, pamoja na huduma za posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto.

Kwa kipindi cha robo mwaka inayoishia Machi 2026, huduma za mawasiliano ya simu zimeonesha ukuaji kukiwa na ongezeko la usajili wa laini wa asilimia 4.6 kutoka milioni 106.9 katika robo mwaka inayoishia Desemba 2025 na kufikia milioni 111.9. Mkoa wa Dar es Salaam imeendelea kuongoza kwa kuwa na laini nyingi za simu kufikia milioni 20.6. Vilevile, usajili wa intaneti umeongezeka kwa asilimia 1.5 kutoka laini milioni 58.1 katika robo mwaka iliyoishia Desemba 2025 na kufikia laini milioni 58.9, na matumizi ya huduma za intaneti yameongezeka kwa asilimia 15.3 kutoka petabytes 808 katika robo mwaka inayoishia Desemba 2025 na kufikia PetaBytes 932. Aidha, idadi ya dakika ndani ya nchi na idadi ya jumbe fupi (SMS) zilipungua kwa asilimia 3.8 na 4.7, mtawalia. Intaneti ya kasi imeendelea kuwa njia inayopendelewa zaidi kupata intaneti ikichangia asilimia 58 ya usajili wote wa intaneti.

Idadi ya simu janja imeongezeka kwa asilimia 4.6 kutoka simu janja milioni 28.5 katika robo mwaka iliyoishia Desemba 2025 kufikia milioni 29.8. Ukuaji huu umechangiwa na upatikanaji wa huduma za mawasiliano kutokana na uendelezwaji wa miundombinu unaodhihirishwa na ongezeko la idadi ya minara kutoka 10,029 katika robo mwaka iliyoishia Desemba 2025 na kufikia minara 10,084.

Katika sekta ya utangazaji, idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa imepungua kwa asilimia 1 kutoka visimbuzi milioni 2.11 katika robo mwaka iliyoishia Desemba 2025 na kufikia visimbuzi milioni 2.09. Aidha, idadi ya televisheni kwa njia ya waya imeongezeka kwa asilimia 3 kutoka televisheni 17,280 katika robo mwaka iliyoishia Desemba 2025 na kufikia televisheni 17,803.

Sekta ya posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto imehudumia jumla ya wateja 170,352 wa kampuni/taasisi na wateja binafsi. Katika kipindi husika, Jumla ya bidhaa za kiposta 546,644 zilitumwa ndani ya nchi na bidhaa 32,565 zilitumwa nje ya nchi. Vilevile, jumla ya bidhaa za kiposta 907,759 zilipokelewa ndani ya nchi na bidhaa 44,555 zilipokelewa kutoka nje ya nchi. Hii inaonesha umuhimu wa sekta ya posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto katika kuwaunganisha wananchi kibiashara.

Sekta bado inakabiliwa na kiwango cha chini cha upenyo wa simu janja cha asilimia 42.5, jambo linalozuia ongezeko la matumizi ya huduma za intaneti ya kasi. Aidha, kuna pengo la asilimia 23.7 katika upatikanaji wa huduma za intaneti ya kasi kijiografia, pamoja na kuwepo kwa majaribio ya ulaghai katika baadhi ya maeneo. Vipaumbele vya sekta vinajumuisha upanuzi wa miundombinu ya mawasiliano ya intaneti ya kasi, kuimarisha matumizi ya huduma za kidijitali, pamoja na kuhakikisha uwepo wa miundombinu ya mawasiliano iliyo salama na yenye ulinzi thabiti.

# Yaliyomo

<b>Orodha ya Vifupisho</b>	<b>5</b>
<b>Orodha ya Maneno</b>	<b>7</b>
<b>Muhtasari wa takwimu za Sekta ya Mawasiliano</b>	<b>10</b>
<b>Huduma za Mawasiliano ya Simu na Intaneti</b>	<b>13</b>
1.1. Idadi ya laini za huduma ya mawasiliano ya simu	13
1.1.1. Aina ya Laini za Simu (P2P na M2M)	14
1.2 Bei za huduma za mawasiliano ya simu	17
1.3. Idadi ya dakika na ujumbe mfupi (SMS) kwa huduma ya mawasiliano ya simu	22
1.4 Kuzuru	28
1.5 Vifaa vya mawasiliano vinavyotumia laini za simu	29
1.6 Mgawanyo wa minara ya mawasiliano ya simu	30
1.7 Mitambo ya kurushia mawimbi ya mawasiliano ya simu na intaneti	32
1.9 Huduma za Intaneti	35
1.10 Huduma za Pesa Mtandao	42
1.11 Ubora wa huduma (QoS)	45
<b>Huduma za Utangazaji</b>	<b>66</b>
2.1. Visimbuzi Vilivyolipiwa	66
2.2. Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya	69
2.3. Ueneaji wa huduma za utangazaji	70
2.4. Utekelezaji wa masharti ya leseni za utangazaji	70
2.5 Leseni za huduma za Utangazaji	75
<b>Huduma za Posta na Usafirishaji wa Vifurushi na Vipeto</b>	<b>77</b>
3.1. Idadi ya masanduku ya posta	77
3.2. Wateja wa huduma za usafirishaji wa vifurushi na vipeto	77

---

3.3. Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa	78
3.4. Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa	80
3.5. Ubora wa huduma za Posta na Usafirishaji wa vifurushi na vipeto	83
3.6. Leseni za huduma ya posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto	84

## **Hitimisho**

**85**

# Orodha ya Vifupisho

Kifupisho	Maelezo
<b>2G</b>	Mtandao wa Simu wa Kizazi cha Pili
<b>3G</b>	Mtandao wa Simu wa Kizazi cha Tatu
<b>4G</b>	Mtandao wa Simu wa Kizazi cha Nne
<b>5G</b>	Mtandao wa Simu wa Kizazi cha Tano
<b>BTS</b>	Kituo cha Msingi cha Mawasiliano ya Simu ya 2G
<b>dBm</b>	Desibeli-miliwati
<b>DStv</b>	Digital Satellite Television
<b>DTH</b>	Moja kwa Moja Nyumbani (Direct to Home)
<b>DTT</b>	Televisheni ya Kidijitali ya Miundombinu ya Ardhini
<b>EA</b>	Afrika Mashariki
<b>eNB</b>	Kituo cha Msingi cha Mawasiliano ya Simu ya 4G
<b>FM</b>	Urekebishaji wa Masafa (Frequency Modulation)
<b>FTP</b>	Itifaki ya Uhamishaji Faili
<b>gNB</b>	Kituo cha Msingi cha Mawasiliano ya Simu ya 5G
<b>HF</b>	Masafa ya Juu
<b>Kbps</b>	Kilobiti kwa Sekunde
<b>M2M</b>	Mawasiliano kati ya Mashine na Mashine
<b>Mbps</b>	Megabiti kwa Sekunde
<b>MBs</b>	Megabaiti
<b>Ms</b>	Milisekunde
<b>P2P</b>	Mawasiliano kati ya mtu na mtu
<b>QoS</b>	Ubora wa Huduma
<b>RoW</b>	Mataifa mengine

Kifupisho	Maelezo
<b>SADC</b>	Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika
<b>SMS</b>	Huduma ya Ujumbe Mfupi
<b>TCRA</b>	Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania
<b>TTCL</b>	Shirika la Mawasiliano Tanzania
<b>TTL</b>	Muda wa kuwa hewani (Time To Live)
<b>TV</b>	Televisheni
<b>TZS</b>	Shilingi ya Tanzania
<b>UHF</b>	Masafa ya Juu Sana
<b>VHF</b>	Masafa ya Juu Zaidi
<b>VSAT</b>	Kituo cha Mawasiliano ya Satelaiti (VSAT) kilichosimikwa ardhini

# Orodha ya Maneno

Na	Kipengele	Maelezo
1	<b>Usajili</b>	Usajili wa laini ya simu ambapo imetumika angalau mara moja (sauti, SMS, data) katika kipindi cha siku 90 zilizopita au visimbuzi vilivyolipiwa kwa ajili ya kupata huduma za utangazaji za televisheni .
2	<b>Teknolojia ya mtandao wa simu za mkononi wa kizazi cha pili (2G)</b>	Teknolojia ya kizazi cha pili ya mawasiliano ya simu za mkononi inayoruhusu mawasiliano ya simu ya sauti, ujumbe mfupi wa maneno na intaneti (data) yenye kasi ya kiwango cha chini.
3	<b>Teknolojia ya mtandao wa simu za mkononi wa kizazi cha tatu (3G)</b>	Teknolojia ya kizazi cha tatu ya mawasiliano ya simu za mkononi inayoruhusu mawasiliano ya simu ya sauti, intaneti (data) ya kasi ya wastani na video.
4	<b>Teknolojia ya mtandao wa simu za mkononi wa kizazi cha nne (4G)</b>	Teknolojia ya kizazi cha nne ya mawasiliano ya simu za mkononi yenye kasi ya juu ya intaneti (data) na kiwango cha chini cha ucheleweshaji na uwezo mkubwa kuliko teknolojia ya 3G.
5	<b>Teknolojia ya mtandao wa simu za mkononi wa kizazi cha tano (5G)</b>	Teknolojia ya kizazi cha tano ya mawasiliano ya simu za mkononi yenye kasi ya juu zaidi ya intaneti (data), kiwango cha chini sana cha ucheleweshaji na uwezo mkubwa wa kuunganisha karibu kila kitu kwa njia ya mtandao.
6	<b>Usajili wa Intaneti yenye kasi kupitia simu za mkononi (Mobile Broadband)</b>	Usajili wa mitandao ya intaneti yenye kasi kupitia simu za mkononi yenye kasi ya angalau 2 Mbps na kuendelea.
7	<b>Huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto</b>	Huduma maalum za posta kwa ajili ya ukusanyaji wa haraka, usafirishaji na uwasilishaji wa vifurushi na vipeto, tofauti na huduma za kawaida za posta.
8	<b>Mfumo wa urushaji wa matangazo ya Televisheni kwa mitambo iliyosimikwa ardhini (DTT)</b>	Ni mfumo wa urushaji wa matangazo ya televisheni kidijitali unaotumia miundombinu ya mawasiliano iliyosimikwa ardhini.

Na	Kipengele	Maelezo
9	<b>Televisheni ya kidigitali kwa njia ya Satelaiti (DTH)</b>	Ni mfumo wa urushaji wa matangazo ya televisheni kidijitali kwa njia ya satelaiti moja kwa moja hadi nyumbani
10	<b>Usajili wa intaneti ya kasi inayotumia vifaa visivyohamishika</b>	Ni usajili wa intaneti yenye kasi isiyohamishika inayotumia teknolojia ya nyaya za faiba, za kawaida, satelaiti au bila kutumia waya (FWA).
11	<b>Ueneaji wa kijiografia</b>	Upeo na mipaka ya eneo la kijiografia ambalo huduma au mtandao fulani unapatikana na unaweza kufikiwa na watumiaji, bila kuzingatia kama huduma hiyo imesajiliwa au inatumika kwa wakati huo.
12	<b>Uwezo wa njia ya mawasiliano ya Kimataifa</b>	Jumla ya uwezo wa vifaa vilivyosimikwa kwa ajili ya kupokea na kusafirisha data kupitia njia za kimataifa za intaneti zinazounganisha nchi na nchi nyingine duniani, unaopimwa kwa kipimo cha biti kwa sekunde (kama Mbps, Gbps au Tbps), bila kujali kiasi cha data kinachopitishwa kwa wakati husika.
13	<b>Ukawiaji katika kusafirisha data</b>	Muda unaohitajika kwa paketi ya data kusafiri kutoka kwenye chanzo hadi sehemu inayopelekwa na kurudi
14	<b>Mawasiliano ya Mashine kwa Mashine (M2M)</b>	Mabadilishano ya moja kwa moja ya taarifa kati ya vifaa au mashine, bila kuingiliwa na binadamu
15	<b>Mawasiliano ya simu nje ya mtandao</b>	Mawasiliano ya simu baina ya wateja kutoka mtandao mmoja wa simu kwenda mtandao mwingine wa simu
16	<b>Mawasiliano ya simu ndani ya mtandao</b>	Mawasiliano ya simu baina ya wateja waliopo ndani ya mtandao mmoja wa simu
17	<b>Mawasiliano kati ya Mtu na Mtu (P2P)</b>	Mawasiliano ya pande mbili kati ya watu binafsi

Na	Kipengele	Maelezo
18	<b>Upenyo wa huduma</b>	Kiwango cha upenyo wa huduma ya Mawasiliano kwa kuzingatia idadi ya watu katika eneo husika
19	<b>Asilimia ya watu wanaofikiwa na huduma fulani ya mawasiliano</b>	Asilimia ya watu katika eneo fulani ambao wanafikiwa huduma fulani ya mawasiliano
20	<b>Ubona wa Huduma (QoS)</b>	Ni kiwango cha jumla cha utendaji wa huduma za mawasiliano
21	<b>Huduma ya Kuzuru</b>	Uwezo wa watumiaji wa huduma za simu za mkononi kutumia simu zao za mkononi (sauti, SMS, data) nje ya eneo la mtandao wao wa nyumbani.
22	<b>Huduma ya kuzuru mitandao ya nchi nyingine</b>	Maana yake ni mtumiaji wa simu ya mkononi kuunganishwa na mtandao mwingine wakati yuko nje ya eneo linalohudumiwa na mtandao wake wa nyumbani.
23	<b>Huduma ya kuzuru mitandao iliyo ndani ya nchi kwa watumiaji wa mitandao ya nchi nyingine</b>	Simu za wateja wageni (waliotembelea) wanaopiga na kupokea simu ndani ya nchi (inbound roaming). Maana yake ni mtumiaji wa simu ya mkononi kutoka mtandao mwingine anapotumia mtandao wako akiwa ndani ya eneo linalohudumiwa na mtandao wako.
24	<b>Laini ya mawasiliano ya simu</b>	Moduli ya Utambulisho wa Mteja (SIM) inayofanya kazi katika mfumo wa mtandao wa simu.
25	<b>Ujumbe mfupi (SMS)</b>	Huduma ya ujumbe mfupi wa maandishi.
26	<b>Faiba nyumbani (FTTH)</b>	Faiba zinazofika moja kwa moja kwenye makazi ya mtumiaji.
27	<b>Faiba ofisini (FTTO)</b>	Faiba zinazofika moja kwa moja kwenye ofisi za kampuni na taasisi mbalimbali

# Muhtasari wa takwimu za Sekta ya Mawasiliano

Idadi ya laini za simu



**111.9** milioni  
4.6% ongezeko

Upenyo wa huduma za mawasiliano



**159.8%**

Idadi ya usajili wa huduma ya intaneti



**58.9** milioni  
1.5% ongezeko

Upenyo wa huduma ya intaneti



**84.2%**

Matumizi ya huduma ya intaneti



**932** PB  
15.3% Ongezeko

Asilimia ya watu iliyofikiwa na huduma ya intaneti ya kasi



**93.94%** **94.32%** **32.83%**  
3G 4G 5G

Simu janja



**29.8** milioni  
4.6% Ongezeko

Upenyo wa simu janja



**42.5%**

Idadi ya dakika za huduma ya sauti ya mawasiliano ya simu



**45.4** bilioni  
3.80% imepungua

Idadi ya dakika za huduma za mawasiliano ya simu kimataifa



47.5 milioni  
6.0% Imepungua

Bei ya data ndani ya kifurushi



2.06 TZS  
Wastani

Bei ya huduma ya sauti ndani ya kifurushi



6.30 TZS Nje ya mtandao  
4.65 TZS Ndani ya mtandao

Idadi ya leseni za Mawasiliano ya huduma za simu



1,884  
3.3% Ongeziko

Idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa



2.09 milioni  
1% Imepungua

Idadi ya televisheni zilizo unganishwa kwa huduma ya waya



17.8 elfu  
3% Ongeziko

Idadi ya leseni za Utangazaji



709  
0.1% Imepungua

Idadi ya bidhaa za kiposta vilivyo tumwa ndani ya nchi



546,644  
1.4% Imepungua

Idadi ya bidhaa za kiposta vilivyo pokelewa ndani ya nchi




907,759  
2.9% ongeziko

idadi ya bidhaa za kiposta vilivyo pokelewa ndani ya nchi kutoka mataifa mengine



44,555  
11.5% punguzo

Idadi ya bidhaa za kiposta vilivyo tumwa nje ya nchi



32,565  
8.3% ongeziko

Idadi ya leseni za huduma za kiposta



144  
3.4% Imepungua

Sura ya kwanza 01

# Huduma za Mawasiliano ya Simu na Intaneti



# Huduma za Mawasiliano ya Simu na Intaneti

Katika kipindi cha robo mwaka husika, idadi ya laini za simu za mkononi na za mezani ilifika milioni 111.9, vilevile dakika bilioni 45.4 za huduma ya sauti zimetumika, SMS bilioni 55.1 zimetumwa na kupokelewa na Petabyte 932 za data zilitumika. Ongezeko hili limechangiwa na ueneaji wa mtandao wa huduma za mawasiliano ya simu na intaneti na kuongezeka kwa upenyo wa simu janja.

## 1.1. Idadi ya laini za huduma ya mawasiliano ya simu

Kufikia Desemba 2025

Kufikia Machi 2026

Milioni 106.9

Milioni 111.9

4.6%



Idadi ya laini za simu iliongezeka kwa asilimia 4.6 kutoka milioni 106.9 katika robo mwaka iliyoishia Desemba 2025 hadi laini milioni 111.9 kufikia robo mwaka iliyoishia Machi 2026. Hii inaonesha kuendelea kuwepo kwa uhitaji wa huduma za mawasiliano. Kati ya laini za simu milioni 111.9, laini za simu za mkononi zilichangia asilimia 99 na laini za simu za mezani zilichangia asilimia 0.1 ya laini zote. Jumla ya idadi ya laini za simu za mkononi na mezani kwa robo mwaka iliyoishia Machi 2026 imeoneshwa kwenye Jedwali 1.1.1

Jedwali 1.1.1: Idadi ya laini za simu za mkononi (P2P na M2M) na mezani

Mwezi	Simu za mkononi	Simu za mezani	Jumla
Januari	108,811,040	111,624	108,922,664
Februari	109,799,887	111,793	109,911,680
Machi	111,795,302	111,933	111,907,235

### 1.1.1. Aina ya Laini za Simu (P2P na M2M)

Laini za simu zimegawanywa kwa matumizi ya watu (P2P) na mashine (M2M). Katika robo mwaka inayoishia Machi 2026, kulikua na ongezeko la asilimia 4.7 kwenye laini za P2P, kama inavyoonyeshwa katika Kielelezo 1.1.1.1. Mgawanyo wa laini za simu za P2P kwa kila mtoa huduma umeoneshwa kwenye Jedwali 1.1.1.1 na mgawanyo wa laini za simu za M2M kwa kila mtoa huduma umeoneshwa kwenye Jedwali 1.1.1.2.

#### Kielelezo 1.1.1.1: Aina ya Laini za Simu (P2P na M2M)



Ukuaji wa usajili wa P2P unaashiria kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya simu

4.7%



Ongezeko la M2M linaashiria maendeleo katika usambaji wa huduma za IoT na otomatiki ya kidijitali.

4.4%

#### Jedwali 1.1.1.1: Idadi ya laini za simu za P2P zilizosajiliwa kwa kila mtoa huduma

Mwezi	Airtel	Halotel	TTCL	Vodacom	Yas	Jumla
Januari	23,421,212	17,714,324	1,752,205	33,728,178	31,164,195	107,780,114
Februari	23,388,041	17,855,496	1,774,538	34,570,964	31,161,620	108,750,659
Machi	23,405,300	18,222,244	1,797,670	35,538,870	31,760,354	110,724,438

#### Jedwali 1.1.1.2: Idadi ya laini za M2M zilizosajiliwa kwa kila mtoa huduma

Mwezi	Airtel	Halotel	TTCL	Vodacom	Yas	Jumla
Januari	339,354	88,020	3,461	628,330	83,385	1,142,550
Februari	344,353	90,520	3,467	637,262	85,419	1,161,021
Machi	346,794	93,520	4,023	648,069	90,391	1,182,797


### 1.1.2 Mgawanyo wa laini za simu kwa kila mtoa huduma

Mgawanyo wa laini za simu kwa kila mtoa huduma kwa robo mwaka iliyoishia Machi 2026 umeoneshwa kwenye Jedwali 1.1.2.1 na mgawanyo wa soko umeoneshwa kwenye Kielelezo 1.1.2.1

### Jedwali 1.1.2: Mgawanyo wa laini za simu kwa kila mtoa huduma

Mwezi	Airtel	Halotel	TTCL	Vodacom	Yas	Jumla
Januari	23,760,566	17,802,344	1,755,666	34,356,508	31,247,580	108,922,664
Februari	23,732,394	17,946,016	1,778,005	35,208,226	31,247,039	109,911,680
Machi	23,752,094	18,315,764	1,801,693	36,186,939	31,850,745	111,907,235

#### Kielelezo 1.1.2.1: Mgawanyo wa laini za simu kwa kila mtoa huduma



Soko la mawasiliano limeendelea kuwa la ushindani ambao ni muhimu katika kuchochea unafuu wa huduma.

### 1.1.3 Idadi ya laini za simu kwa kila mkoa na jinsia

#### Kielelezo 1.1.4: Idadi ya laini za simu (P2P) kwa kila jinsia




**56,912,362**  
Wanaume



**53,812,076**  
Wanawake

Wanawake, ambao ni wengi zaidi kuliko wanaume kwa idadi ya watu, wako nyuma kidogo katika matumizi ya huduma za mawasiliano. Kwa upande mwingine, Dar es Salaam ilishika nafasi ya kwanza kwa kuwa na laini milioni 20.60, Mwanza ilishika nafasi ya pili kwa kuwa na laini milioni 7.41, Arusha ilishika nafasi ya tatu kwa kuwa na laini milioni 6.74, Mbeya ilishika nafasi ya nne ikiwa na laini milioni 6.44, na Dodoma ilishika nafasi ya tano kwa kuwa na laini milioni 5.97. Mgawanyo wa idadi ya laini za simu kwa kila mkoa imeoneshwa kwenye Kielelezo 1.1.3.2.


**Kielelezo 1.1.3.2: Idadi ya laini za simu za mkononi na mezani kwa kila mkoa**




### 1.1.4 Mwenendo wa Idadi ya Laini za Simu na Upenyo

Mwenendo wa idadi ya laini za simu ulichangia ongezeko la upenyo kwa robo mwaka. Upenyo ulikua kwa wastani wa asilimia 5.3 katika robo nne za mwaka zilizopita na laini za simu zilikuwa kwa asilimia 6.5 katika kipindi cha marejeo.

**Kielelezo 1.1.4.1: Mwenendo wa Kiwango cha Upenyo wa Mawasiliano ya Simu kwa Robo ya Mwaka**



**Kielelezo 1.1.4.2: Mwenendo wa Usajili wa Laini kwa Robo ya Mwaka**







## 1.2 Bei za huduma za mawasiliano ya simu

Bei za huduma za mawasiliano ya simu zinajumuisha bei nje ya kifurushi na ndani ya kifurushi, zikitozwa kwa dakika, SMS, na data kwa MB kwa matumizi ya ndani ya nchi, Afrika Mashariki (EA) na mataifa mengine (RoW).

### 1.2.1 Bei za huduma za mawasiliano ya simu nje ya kifurushi

Katika robo mwaka iliyoishia Machi 2026, bei zinazotuzwa kwa huduma za data, sauti kwa dakika na huduma za SMS kwa matumizi ya nchini, EA na RoW hazikubadilika, kama inavyoonyeshwa katika Kielelezo 1.2.1.1.

### Kielelezo 1.2.1.1: Bei (Tsh) za huduma za mawasiliano ya simu

	Desemba 2025	Machi 2026	Badiliko
 Ndani ya mtandao	29.00	29.00	0.0%
	Nje ya mtandao	29.00	0.0%
 SMS kitaifa	8.10	8.10	0.0%
	SMS Kimataifa	189.61	189.61
 Afrika Mashariki	247.52	247.52	0.0%
	Mataifa mengine	2,315.82	2,315.82
 Data	9.35	9.35	0.0%

#### 1.2.1.1 Bei za Huduma ya Sauti (Tsh)

Hizi ni bei za huduma ya sauti kwa dakika moja ya kupiga simu ndani ya nchi au kimataifa bila kujiunga kwenye kifurushi. Bei za huduma ya sauti kwa robo ya mwaka inayoishia Machi 2026 kwa simu za ndani na nje ya nchi kwa kila mtoa huduma zimeoneshwa kwenye Jedwali 1.2.1.1.1.

#### Jedwali 1.2.1.1.1: Bei (Tsh) za kupiga simu ndani na nje ya nchi kwa kila mtoa huduma

Mtoa Huduma	Ndani ya mtandao	Nje ya mtandao	Afrika mashariki	Mataifa mengine
Airtel	30.00	30.00	260.00	2,350.00
Halotel	25.00	25.00	250.00	1,424.44
Yas	30.00	30.00	260.00	2,550.00
TTCL	30.00	30.00	217.60	2,871.33
Vodacom	30.00	30.00	250.00	2,383.33
<b>Wastani</b>	<b>29.00</b>	<b>29.00</b>	<b>247.52</b>	<b>2,315.82</b>

Jedwali 1.2.1.1.1 linaonesha kuwa hakuna tofauti ya bei za kupiga simu ndani na nje ya mtandao. Wakati watoa huduma wote walitoza Tsh 30 kwa dakika ndani na nje ya mtandao, Halotel alitoza Tsh 25 kwa dakika. Aidha, bei za kupiga simu Kwenda Afrika Mashariki (EA) na mataifa mengine (RoW) zilikuwa tofauti kwa kila mtoa huduma. Wastani wa bei ya huduma ya sauti ndani ya nchi, EA na RoW katika robo mwaka iliyoishia Machi 2026 ulibakia kama ilivyokuwa katika robo mwaka iliyoishia Desemba 2025.

### 1.2.1.2 Bei za SMS na Data (Tsh)

Wastani wa bei ya kutuma SMS ndani na nje ya nchi bila kujiunga kwenye kifurushi, pamoja na bei ya data katika robo mwaka iliyoishia Machi 2026 ulibaki kama ulivyokuwa katika robo mwaka iliyoishia Desemba 2025. Wastani wa bei ya SMS ndani na nje ya nchi, na data umeoneshwa katika Jedwali 1.2.1.2.1

#### Jedwali 1.2.1.2.1: Bei (Tsh) za SMS na data

Mtoa huduma	SMS kitaifa	SMS kimataifa	Data /MB
Airtel	8.00	215.00	9.35
Halotel	6.50	95.00	9.35
Yas	8.00	215.00	9.35
TTCL	10.00	138.06	9.35
Vodacom	8.00	285.00	9.35
<b>Wastani</b>	<b>8.10</b>	<b>189.61</b>	<b>9.35</b>

### 1.2.2 Bei za Huduma za Mawasiliano ya Simu Katika Vifurushi (Tsh)

Bei za huduma za mawasiliano ya simu ndani ya kifurushi kwa dakika, SMS na data (MB) zimebadilika kwa viwango tofauti katika robo ya mwaka inayoishia Machi 2026 ikilinganishwa na robo ya mwaka inayoishia Desemba 2025, kama inavyooneshwa katika Jedwali 1.2.2.1.

#### Jedwali 1.2.2.1: Bei (Tsh) za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi

Kipindi	Ndani ya mtandao	Nje ya mtandao	SMS	Data
Machi 2026	4.65	6.30	1.45	2.06
Desemba 2025	5.11	6.33	1.44	2.06
<b>Badiliko</b>	<b>-9.0%</b>	<b>-0.5%</b>	<b>0.7%</b>	<b>0.0%</b>

### Jedwali 1.2.2.2: Bei (Tsh) za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi kwa kila mtoa

Kipindi	Ndani ya mtandao	Nje ya mtandao	SMS	Data
Airtel	2.05	7.60	1.18	2.05
Halotel	4.51	5.07	1.54	2.05
Yas	5.36	6.11	1.22	2.04
TTCL	6.80	6.80	2.07	2.08
Vodacom	4.55	5.92	1.22	2.10
<b>Wastani</b>	<b>4.65</b>	<b>6.30</b>	<b>1.45</b>	<b>2.06</b>

Jedwali 1.2.2.2 linaonesha kuwa watoa huduma walitoza bei kwa viwango tofauti katika huduma za mawasiliano ya simu.

### 1.2.3 Wastani wa Bei (Tsh) za Huduma za Mawasiliano ya Simu

Wastani wa bei za huduma ya mawasiliano ya simu ndani na nje ya kifurushi katika kipindi cha marejeo unaonesha kuwa bei ndani ya kifurushi ni ndogo ikilinganishwa na bei nje ya kifurushi, kama inavyooneshwa katika Jedwali 1.2.3.1. Unafuu wa bei za huduma za mawasiliano ya simu ndani ya kifurushi unasababisha watumiaji wengi (99.9%) kupendelea kujiunga na huduma za vifurushi.


#### Jedwali 1.2.3.1: Wastani wa bei (Tsh) za huduma za mawasiliano ya simu

	Ndani ya mtandao	Nje ya mtandao	SMS	Data
Wastani bila kifurushi	29.00	29.00	8.10	9.35
Wastani katika kifurushi	4.65	6.30	1.45	2.06


#### 1.2.3.1 Mwenendo wa Wastani wa Bei za Huduma za Mawasiliano ya Simu

Mwenendo wa wastani wa bei za huduma za sauti, SMS na data ndani na nje ya kifurushi, kitaifa na kimataifa katika kipindi cha robo mwaka umeoneshwa kwenye kielelezo 1.2.3.1.1, 1.2.3.1.2, 1.2.3.1.3, na 1.2.3.1.4. Bei za nje ya kifurushi kwa huduma za sauti, SMS na data hazikuwa na mabadiliko katika robo mwaka tatu mfululizo.


**Kielelezo 1.2.3.1.1: Mwenendo wa Wastani wa Bei ya Huduma ya Sauti nje ya kifurushi kwa robo mwaka**




**Kielelezo 1.2.3.1.2: Mwenendo wa Wastani wa Bei ya Huduma ya Sauti Kimataifa kwa robo mwaka**



**Kielelezo 1.2.3.1.3: Mwenendo wa Wastani wa Bei ya Huduma ya SMS nje ya kifurushi kwa robo mwaka**



**Kielelezo 1.2.3.1.4: Mwenendo wa Wastani wa Bei ya Huduma za mawasiliano ya simu ndani ya kifurushi kwa robo mwaka**



### 1.3. Idadi ya dakika na ujumbe mfupi (SMS) kwa huduma ya mawasiliano

Katika kipindi cha marejeo, takwimu zinaonesha kuendelea kuwepo kwa mahitaji ya huduma za mawasiliano ambapo dakika bilioni 45.4 zilitumika kwa simu za ndani ya nchi na milioni 207.3 zilitumika kwa simu za kimataifa. Kwa upande mwingine, SMS bilioni 55.1 zilitumwa na kupokelewa ndani ya nchi, na SMS milioni 3.1 zilitumwa na kupokelewa kimataifa.



#### 1.3.1 Idadi ya dakika za huduma ya sauti

##### 1.3.1.1 Idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani ya nchi



Idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani na nje ya mtandao ilipungua kwa asilimia 3.8 katika kipindi cha marejeo kama ilivyooneshwa kwenye kielelezo hapo juu. Uchambuzi unaonesha kuwa idadi ya dakika ndani ya mtandao na nje ya mtandao ilipungua kwa asilimia 7.10 na 0.10, mtawalia, kama ilivyooneshwa katika Kielelezo 1.3.1.1. Aidha, Jedwali 1.3.1.1 linaonesha kuwa mwezi Januari ulikuwa na dakika nyingi zaidi ikilinganishwa na Februari na Machi.

**Kielelezo 1.3.1.1: Idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani na nje ya mtandao ndani ya nchi**


	Robo mwaka iliyoishia Desemba 2025	Robo mwaka iliyoishia Machi 2025	Badiliko
Ndani ya mtandao	<b>Bilioni 24.70</b>	Bilioni 22.95	7.10% 
Nje ya mtandao	<b>Bilioni 22.51</b>	Bilioni 22.49	0.10% 

**Jedwali 1.3.1.1: Idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani na nje ya mtandao nchini**


	Januari	Februari	Machi
Ndani ya mtandao	8,004,814,102	7,107,671,501	7,837,852,021
Nje ya mtandao	7,905,974,576	6,955,913,140	7,628,733,376
<b>Jumla</b>	<b>15,910,788,678</b>	<b>14,063,584,641</b>	<b>15,466,585,397</b>

Mgawanyo wa dakika ndani na nje ya mtandao nchini kwa kila mtoa huduma umeoneshwa kwenye Kielelezo 1.3.1.2 na 1.3.1.3. Airtel iliongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya dakika za ndani ya mtandao (34.3%) na nje ya mtandao (29.6%). Aidha, mwenendo wa idadi (Milioni) ya dakika za huduma ya sauti ndani ya nchi kwa robo mwaka imeoneshwa kwenye Kielelezo 1.3.1.4


**Kielelezo 1.3.1.2: Mgawanyo wa dakika za huduma ya sauti ndani ya mtandao kwa kila mtoa huduma**




**Kielelezo 1.3.1.3: Mgawanyo wa dakika za huduma ya sauti nje ya mtandao kwa kila mtoa huduma**



**Kielelezo 1.3.1.4: Mwenendo wa idadi (Milioni) ya dakika za huduma ya sauti ndani ya nchi kwa robo mwaka**



### 1.3.1.2 Idadi ya dakika za huduma ya sauti nje ya nchi



Kielelezo kinaonesha kuwa idadi ya dakika kwenda nje ya nchi imeongezeka kwa asilimia 4 na dakika kutoka nje ya nchi imepungua kwa asilimia 6. Vilevile, takwimu zinaonesha kuwa asilimia 77 ya dakika za sauti zilizotumika kimataifa zilitokana na simu kwenda nje ya nchi, wakati asilimia 23 zilitokana na simu zilizoingia kutoka nje ya nchi.


Jumla ya dakika kwenda na kutoka EA, SADC na RoW kwa robo mwaka iliyoishia Machi 2026 imeoneshwa katika Jedwali 1.3.1.2.1. Aidha, mgawanyo wa dakika kwenda na kutoka EA, SADC na RoW umeoneshwa kwenye Kielelezo 1.3.1.2.1, 1.3.1.2.2 na 1.3.1.2.3, mtawalia. Kwa ujumla, dakika nyingi za simu za kimataifa ni za kutoka na kwenda ukanda wa EA ikilinganishwa na SADC na RoW.

**Jedwali 1.3.1.2.1: Idadi ya dakika za huduma ya sauti kwenda na kutoka EA, SADC na RoW**

Mwezi	Januari	Februari	Machi	Jumla
Kwenda EA	52,944,689	49,530,044	54,903,517	157,378,250
Kutoka EA	14,696,155	13,450,500	14,420,228	42,566,883
Kwenda SADC	102,026	88,166	89,161	279,353
Kutoka SADC	180,435	178,085	175,416	533,936
Kwenda RoW	763,681	690,467	703,639	2,157,787
Kutoka RoW	1,475,722	1,347,393	1,537,881	4,360,996


### Kielelezo 1.3.1.2.1 Mgawanyo wa dakika za huduma ya sauti kwenda na kutoka EA

■ Kwenda EA ■ Kutoka EA




### Kielelezo 1.3.1.2.2: Mgawanyo wa dakika za huduma ya sauti kwenda na kutoka SADC

■ Kwenda SADC ■ Kutoka SADC



### Kielelezo 1.3.1.2.3 Mgawanyo wa dakika za huduma ya sauti kwenda na kutoka RoW

■ Kwenda RoW ■ Kutoka RoW



## 1.3.2 Idadi ya SMS

### 1.3.2.1 Idadi ya SMS kitaifa

Muhtasari unaonesha kuwa idadi ya SMS ilipungua kwa asilimia 4.7 katika robo mwaka iliyoishia Machi 2026

Kufikia Desemba 2025

**Bilioni 57.8**

Kufikia Machi 2026

**Bilioni 55.1**

**4.7%**



**Jedwali 1.3.2.1.1: Idadi ya dakika za huduma ya SMS ndani na nje ya mtandao**


Kipindi	SMS ndani ya mtandao	SMS nje ya mtandao	Jumla
Machi 2026	Bilioni 22.61	Bilioni 32.47	Bilioni 55.08
Desemba 2025	Bilioni 24.20	Bilioni 33.61	Bilioni 57.80
<b>Badililiko</b>	<b>-6.54%</b>	<b>-3.39%</b>	<b>-4.71%</b>

Idadi ya SMS ndani na nje ya mtandao ilipungua kwa asilimia 6.54 na 3.39, mtawalia, kwa kipindi husika kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali 1.3.2.1.1. Aidha, Jedwali 1.3.2.1.2 linaonesha kuwa Januari ilikuwa na idadi kubwa zaidi ya SMS ikilinganishwa na mwezi Februari na Machi. Aidha, mwenendo wa idadi (Bilioni) ya SMS ndani ya nchi kwa robo mwaka imeoneshwa kwenye Kielelezo 1.3.2.1.1

**Jedwali 1.3.2.1.2: Idadi ya dakika za huduma ya SMS ndani na nje ya mtandao kwa robo mwaka iliyoishia Machi 2026**

Kipindi	Januari	Februari	Machi	Jumla
SMS ndani ya mtandao	8,137,633,126	6,868,724,329	7,606,701,869	22,613,059,324
SMS nje ya mtandao	11,695,855,033	9,771,932,712	11,002,616,884	32,470,404,629
<b>Jumla</b>	<b>19,833,488,159</b>	<b>16,640,657,041</b>	<b>18,609,318,753</b>	<b>55,083,463,953</b>

**Kielelezo 1.3.2.1.1: Mwenendo wa idadi ya SMS za ndani ya nchi kwa robo mwaka**




### 1.3.2.2 Idadi ya SMS kimataifa

Idadi ya SMS kwenda na kutoka EA, SADC na RoW katika robo mwaka iliyoishia Machi 2026 imeoneshwa kwenye Jedwali 1.3.2.2.1. Vilevile, mgawanyo wa idadi ya SMS kwenda na kutoka EA, SADC na RoW umeoneshwa kwenye Kielelezo 1.3.2.2.1, 1.3.2.2.2 na 1.3.2.2.3, mtawalia. Kwa ujumla kulikuwa na SMS nyingi kutoka RoW ikilinganishwa na SMS kutoka EA na SADC.


**Kielelezo 1.3.2.2.1: Mgawanyo wa SMS kwenda na kutoka EA**

■ Kwenda EA ■ Kutoka EA




**Kielelezo 1.3.2.2.2: Mgawanyo wa SMS kwenda na kutoka SADC**

■ Kwenda SADC ■ Kutoka SADC



**Kielelezo 1.3.2.2.3: Mgawanyo wa SMS kwenda na kutoka RoW**

■ Kwenda RoW ■ Kutoka RoW



### Jedwali 1.3.2.2.1: Idadi ya SMS kwenda na kutoka EA, SADC na RoW

	Januari	Februari	Machi	Jumla
Kwenda EA	66,321	51,532	57,273	175,126
Kutoka EA	169,960	135,890	149,752	455,602
Kwenda SADC	21,095	17,400	18,126	56,621
Kutoka SADC	119,866	110,284	112,001	342,151
Kwenda RoW	452,037	361,045	405,079	1,218,161
Kutoka EA	430,236	272,830	140,348	843,414

## 1.4 Kuzuru

Katika robo mwaka husika, idadi ya dakika za sauti na SMS kwa huduma ya kuzuru-kwenda ilikuwa kubwa ikilinganishwa na kuzuru-kutoka. Kwa upande mwingine, idadi ya data (PB) kwa huduma ya kuzuru-kwenda ilikuwa ndogo ikilinganishwa na ya kuzuru-kutoka kama inavyooneshwa kwenye kielelezo 1.4. Vilevile, takwimu zinaonesha kuwa kuna pengo kubwa kati ya idadi ya data (PB) kwa huduma ya kuzuru-kwenda na kuzuru-kutoka.

### Kielelezo 1.4: Kuzuru

	Dakika	SMS	Data
Kuzuru-kwenda	<b>Bilioni 6.6</b>	<b>Milioni 6.0</b>	<b>PB 6,263.6</b>
Kuzuru-Kutoka	<b>Bilioni 1.2</b>	<b>Milioni 0.9</b>	<b>PB 207,600</b>

### 1.4.1 Kuzuru Huduma ya Sauti (Dakika)

Idadi ya dakika kwa huduma ya kuzuru ya sauti kutoka na kwenda EA, SADC na RoW kwa robo mwaka iliyoishia Machi 2026 imeoneshwa kwenye jedwali 1.4.1.1.

#### Jedwali 1.4.1.1: Kuzuru huduma ya sauti (dakika)

	EA	SADC	RoW	Jumla
Kuzuru kwenda	13,328,977	40,319	6,610,990,931	6,624,360,227
Kuzuru kutoka	892,935,699	4,301,715	284,399,088	1,181,636,502

### 1.4.2 Kuzuru huduma ya SMS

Idadi ya SMS kutoka na kwenda EA, SADC na RoW kwa huduma za kuzuru kwa robo mwaka iliyoishia Machi 2026 imeoneshwa kwenye jedwali 1.4.2.1.

**Jedwali 1.4.2.1: Kuzuru huduma ya SMS**

	EA	SADC	RoW	Jumla
Kuzuru kwenda	3,067,286	504,455	2,429,198	6,000,939
Kuzuru kutoka	259,530	71,883	597,599	929,012

### 1.4.3 Kuzuru huduma ya intaneti

Idadi ya megabaiti kutoka na kwenda EA, SADC na RoW kwa huduma za kuzuru kwa robo mwaka iliyoishia Machi 2026 imeoneshwa kwenye jedwali 1.4.3.1.

**Jedwali 1.4.3.1: Kuzuru huduma ya intaneti (MB)**

	EA	SADC	RoW	Jumla
Kuzuru kwenda	3,212,006	1,193,959	6,263,616,346,868	6,263,620,752,833
Kuzuru kutoka	4,450,629,908,713	4,876,786,821,712	198,272,490,254,587	207,599,906,985,012

## 1.5 Vifaa vya mawasiliano vinavyotumia laini za simu

Upenyo wa simu janja uliongezeka kutoka asilimia 41.82 katika robo mwaka iliyoishia Desemba 2025 na kufikia asilimia 42.5 katika robo mwaka iliyoishia Machi 2026. Vilevile, upenyo wa simu rununu umepungua kutoka asilimia 87.1 na kufikia asilimia 83.6 kama inavyooneshwa katika Kielelezo 1.5.1.

**Kielelezo 1.5.1: Upenyo wa simu za mkononi**

Simu janja



**42.5%**

Upenyo

Simu rununu



**83.6%**

Upenyo

Asilimia kubwa ya vifaa vinavyotumia laini ni simu rununu

Licha ya ongezeko la upenyo wa vifaa vya mawasiliano, upenyo wa simu janja bado upo chini ukilinganishwa na ueneaji wa mtandao. Hii inaashiria kuwepo kwa fursa za uwekezaji wa kimkakati kwenye vifaa vya bei nafuu ili kusaidia kupunguza ombwe la kidijitali. Vifaa vingine vya mawasiliano kama vile Handheld, Modem, na Tablets vina upenyo wa chini ya asilimia 6 kama inavyooneshwa katika Jedwali 1.5.1.

### Jedwali 1.5.1: Vifaa vya mawasiliano vinavyotumia laini za simu na kuunganishwa


Aina ya kifaa	Idadi ya vifaa	Upenyo
Mobile Phone/Feature phone	58,557,316	83.61%
Smartphone	29,799,766	42.55%
Handheld	1,360,055	1.94%
Modem	799,934	1.14%
Tablet	514,720	0.73%
WLAN Router	569,917	0.81%
IoT Device	186,780	0.27%
Module	82,433	0.12%
Dongle	78,886	0.11%
Portable(include PDA)	71,035	0.10%
Connected Computer (with SIM card slot)	14,924	0.02%
Wearable	14,950	0.02%
Vehicle	7,062	0.01%
Device for the Automatic Processing of Data (APD)	4,409	0.01%
Others	4,890	0.01%
e-Book	26	0.00%
Mobile Test Platform	2	0.00%

### 1.6 Mgawanyo wa minara ya mawasiliano ya simu

Ueneaji wa minara ya mawasiliano ya simu unalenga kuwafikia wale ambao bado hawajafikiwa na huduma na kupunguza pengo la kidijiti. Hii inahakikishwa na uwepo wa miundombinu imara, jumuishi, rafiki kwa mazingira na iliyo tayari kwa mahitaji ya baadaye. Hali inaonesha kuwa minara imejengwa katika mikoa yote ili kuhakikisha huduma zinapatikana katika maeneo yote yenye makazi ya watu.

Katika kipindi husika, kulikuwa na minara 10,084 na Dar es Salaam ikiongoza kwa kuwa na minara 1,242. mgawanyo wa minara ya mawasiliano kwa kila mkoa, kama inavyoonyeshwa katika Kielelezo 1.6.1, unachochea idadi ya watu pamoja na shughuli za kiuchumi.


**Kielelezo 1.6.1: Mgawanyo wa minara ya mawasiliano ya simu kimkoa**



## 1.7 Mitambo ya kurushia mawimbi ya mawasiliano ya simu na intaneti

Uwekaji wa mitambo ya kurushia mawimbi ya simu nchini umekuwa ni msingi katika uunganishaji wa mtandao. Kielelezo 1.7.1 kinaonesha teknolojia ya 2G, 3G na 4G, ikiwa na BTS 15,742, NodeB 14,521 na eNB 15,464. Vilevile, ueneaji wa teknolojia ya 5G umeongezeka kwa asilimia 44 na kufikia gNBs 1,804.

**Kielelezo 1.7.1: Mgawanyo wa Mitambo ya kurushia mawimbi kwa Teknolojia**



Dar es Salaam inaongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya mitambo ya kurushia mawimbi ya mawasiliano kwa teknolojia zote (2G, 3G, 4G na 5G), na kuifanya kuwa kitovu cha mawasiliano nchini, kama inavyooneshwa kwenye Jedwali 1.7.1. ambalo linaonesha mgawanyo wa mitambo ya kurushia mawimbi ya mawasiliano kimkoa.



### Jedwali 1.7.1: Mgawanyo wa mitambo ya kurushia mawimbi ya simu kimkoa

Mkoa	Idadi ya mitambo ya kurushia			
	(2G)	NodeB (3G)	eNB (4G)	gNB (5G)
<b>Tanzania bara</b>				
Arusha	781	730	765	78
Dar-es-salaam	2,453	2,406	2,536	1,121
Dodoma	799	664	780	94
Geita	463	447	465	15
Iringa	444	392	438	17
Kagera	573	558	565	6
Katavi	195	179	189	8
Kigoma	509	507	512	8
Kilimanjaro	602	563	582	16
Lindi	380	291	348	7
Manyara	389	310	357	5
Mara	447	437	445	8
Mbeya	645	614	639	53
Morogoro	814	706	801	31
Mtwara	460	377	427	6
Mwanza	789	792	797	93
Njombe	349	292	338	6
Pwani	602	518	591	31
Rukwa	307	297	296	4
Ruvuma	467	373	418	8
Shinyanga	421	414	420	17
Simiyu	320	312	311	5
Singida	390	343	372	7
Songwe	266	254	253	19
Tabora	592	564	582	12
Tanga	672	576	623	14
<b>Zanzibar</b>				
Kaskazini Pemba	67	65	62	3
Kaskazini Unguja	97	92	95	5
Kusini Pemba	73	72	71	4
Kusini Unguja	109	105	110	8
Mjini Magharibi	267	271	276	95
<b>Jumla</b>	<b>15,742</b>	<b>14,521</b>	<b>15,464</b>	<b>1,804</b>

## 1.8 Ueneaji wa miundombinu ya mawasiliano

Uwekezaji katika miundombinu ya mawasiliano umeongeza usambaji wa huduma ya mawasiliano. Kumekuwa na ongezeko la ueneaji wa mtandao wa 5G ulioongezeka kufikia asilimia 11.04 na 32.83 kijiografia na kwa idadi ya watu, mtawalia, katika kipindi husika, kama ilivyooneshwa katika Jedwali 1.8.1.

Jedwali 1.8.1: Ueneaji wa miundombinu ya mawasiliano

		Desemba 2025	Machi 2026
 <b>Asilimia ya watu waliofikiwa na huduma ya mawasiliano</b>	<b>2G</b>	98.64%	98.65%
	<b>3G</b>	93.92%	93.94%
	<b>4G</b>	94.21%	94.32%
	<b>5G</b>	30.13%	32.83%
 <b>Asilimia ya eneo lilofikiwa na huduma ya mawasiliano</b>	<b>2G</b>	79.47%	79.62%
	<b>3G</b>	76.18%	76.31%
	<b>4G</b>	77.31%	77.43%
	<b>5G</b>	10.54%	11.04%

## 1.9 Huduma za Intaneti

Kumekuwa na ongezeko la idadi ya utumiaji wa Intaneti la asilimia 1.5 na ongezeko la matumizi ya Intaneti la asilimia 15.3 katika robo mwaka iliyoishia Machi 2026. Ongezeko hilo linaonesha mahitaji endelevu ya huduma ya intaneti ya kasi. Vilevile, idadi ya utumiaji wa Intaneti inaoneshwa kwenye jedwali 1.9.1.

### 1.9.1 Utumiaji wa Intaneti

Kufikia Desemba 2025

Milioni 58.1

Kufikia Machi 2026

Milioni 58.9

1.5% 

Jedwali 1.9.1.1: Idadi ya utumiaji wa Intaneti kwa robo ya mwaka inayoishia Machi 2026


Mwezi	Mobile Wireless	Fixed Wireless	Fixed Wired	Jumla
Januari	57,831,937	303,688	150,866	58,286,491
Februari	57,683,071	325,431	163,476	58,171,978
Machi	58,466,927	347,400	160,493	58,974,820
<b>Upenyo</b>				<b>84.20%</b>

Intaneti ya kasi kwa huduma ya simu ndiyo njia inayopendelewa zaidi kupata Intaneti, ikiwa na laini 34,283,024. Teknolojia ya 2G bado ina matumizi makubwa, ikiwa na laini 24,183,903. Teknolojia za Faiba Nyumbani (Fiber to the Home - FTTH) na Faiba Ofisini (Fiber to the Office - FTTO) zina idadi ndogo ya usajili ikilinganishwa na njia ya simu za mkononi kama inaovyooneshwa katika Kielelezo 1.9.1.1.

Jedwali 1.9.1.2: Usajili wa kasi ya intaneti kwa huduma ya intaneti wa miundombinu isiyohamishika


kasi ya intaneti kwa huduma ya intaneti wa miundombinu isiyohamishika	Usajili
< 256 Kbps	10
>= 256 Kbps < 2Mbps	1,466
>= 2Mbps < 10Mbps	63,407
>= 10Mbps < 30Mbps	281,346
>= 30Mbps < 100Mbps	146,771
>= 100Mbps < 1Gbps	14,158
>= 1Gbps	735
<b>Jumla</b>	<b>507,893</b>

**Kielelezo 1.9.1.1: Utumiaji wa Intaneti kwa teknolojia**




Soko la huduma ya intaneti ya miundombinu inayohamishika limeendelea kuonesha ushindani mkubwa ambao ni muhimu katika kuchochea unafuu wa bei ya huduma.

**Kielelezo 1.9.1.2: Mgawanyo wa huduma ya Intaneti kwa njia ya simu kwa kila mtoa huduma kwa robo mwaka inayoishia Machi 2026**



Soko la huduma ya intaneti ya miundombinu isiyohamishika limeonesha kuongezeka kwa matumizi ya huduma kama inavyoonekana kwenye kielelezo 1.9.1.3.

### Kielelezo 1.9.1.3: Idadi ya laini za intaneti (fixed) kwa kila mtoa huduma




Usajili wa laini za Intaneti (fixed)  
kwa watu binafsi ni **404,050**



Usajili wa laini za Intaneti (fixed)  
kwa Taasisi ni **103,843**

## 1.9.2 Matumizi ya huduma ya Intaneti

Matumizi ya intaneti yanaakisi jumla ya kiwango cha utumiaji wa data katika robo mwaka husika. Kielelezo hapo chini kinaonesha kuwa kiwango cha matumizi kimeongezeka kwa asilimia 15.3 ikilinganishwa na robo mwaka iliyopita. Vilevile, wastani wa kiashiria cha ubora wa huduma ya intaneti kwa ukawiaji (ms) ilikuwa ni 68.85 kwa maeneo kumi na tisa yaliyopimwa kama inavyooneshwa kwenye Jedwali 1.9.2



**Jedwali 1.9.2.1: Kiashiria cha ubora wa huduma ya intaneti kwa ukawiaji (ms) kwa maeneo yaliyopimwa**

Maeneo yaliyopimwa	Airtel	Halotel	Yas	TTCL	Vodacom	Wastani
Arusha	47.1	73.1	98.4	67.6	51.4	67.51
Ilala	83.1	61.2	63.8	51.7	41.3	60.21
Kigamboni	78.6	64.7	67.6	54.3	53.1	63.65
Kinondoni	72.7	53.3	72.6	58.6	36.3	58.69
Temeke	70.7	65.5	65.3	66.2	66.7	66.86
Ubungo	145.5	61.8	68.8	52.5	53.8	76.49
Iringa	55.4	69.4	96.4	73.3	43.7	67.62
Kilimanjaro	42.7	60.5	108.7	72.2	59.2	68.64
Mara	51.9	56.3	87.4	104.0	54.7	70.86
Mbeya	75.9	111.4	59.6	95.0	53.4	79.06
Morogoro	95.7	51.4	84.4	72.4	45.0	69.77
Mtwara	56.1	56.9	78.7	61.0	57.7	62.06
Mwanza	63.3	77.7	87.8	89.9	59.2	75.59
Njombe	49.0	71.8	84.6	66.0	57.9	65.87
Pemba	109.6	115.6	50.6	63.2	63.9	80.56
Shinyanga	57.4	54.2	99.8	77.0	53.9	68.44
Simiyu	64.4	53.6	111.7	70.9	57.0	71.52
Tanga	51.9	59.7	86.5	86.8	45.5	66.09
Unguja	112.1	68.8	48.7	63.7	50.0	68.65
<b>Wastani</b>						<b>68.85</b>

**Jedwali 1.9.2.1: Kiasi cha data kilichotumika kwa teknolojia inayohamishika katika robo ya mwaka inayoishia Machi 2026**

	Januari	Februari	Machi
GB	144,373,420	139,503,183	146,949,030
Usajili wa intaneti	57,831,937	57,683,071	58,466,927
Kiasi cha data kwa kila usajili	2.50	2.42	2.51

Jedwali 1.9.2.1 linaonesha kuwa GB 2.51 kwa kila usajili wa huduma ya intaneti kwa teknolojia inayohamishika imetumika mwezi Machi 2026 ambayo ni kubwa kuliko Januari na Februari 2026. Aidha, kwa kila usajili wa huduma ya intaneti kwa teknolojia isiyohamishika imeoneshwa kwenye jedwali 1.9.2.2 na matumizi ya data kwa kila programu ya OTT kwa majukwaa ya mitandao ya kijamii yameoneshwa kwenye Jedwali 1.9.2.3

**Table 1.9.2.2: Kiasi cha utumiaji wa data kwa teknolojia ya Intaneti isiyohamishika katika robo ya mwaka inayoishia Machi 2026**

	Januari	Februari	Machi
GB	157,927,373	148,722,206	173,096,285
Usajili wa intaneti	454,554	488,907	507,893


**Jedwali 1.9.2.3: Matumizi ya data kwa kila programu ya OTT kwa majukwaa ya mitandao ya kijamii**

Jina la Programu	Matumizi (GB)	Nafasi
YouTube	80,319	1
Tik Tok	72,097	2
Facebook	67,608	3
Instagram	35,361	4
WhatsApp	29,074	5
Snapchat	10,548	6
WeChat	7,972	7
Pinterest	992	8
Microsoft Teams	565	9
Linkedin	342	10

Ongezeko la utumiaji wa intaneti na matumizi ya data unaashiria uwepo wa fursa katika maeneo tofauti mathalani, uwekezaji kwenye intaneti ya kasi na huduma za kidijiti.

### 1.9.3 Wastani wa kasi na ukawiaji wa intaneti

Wastani wa kasi ya kupakua na kupakia imeoneshwa kwenye kielelezo 1.9.3, huku, kiashiria cha kasi ya kupakua (Mbps) kwa maeneo yaliyopimwa robo mwaka iliyoishia Machi 2026 imeoneshwa kwenye jedwali 1.9.3.1.



**Jedwali 1.9.3.1: Kiashiria cha kasi ya kupakua (Mbps) kwa maeneo yaliyopimwa robo mwaka iliyoishia Machi 2026**

Eneo la upimaji	Airtel	Halotel	Yas	TTCL	Vodacom	Wastani
Arusha	20.0	9.9	21.2	17.9	16.7	17.13
Ilala	19.1	4.6	13.5	17.5	19.4	14.82
Kigamboni	17.6	9.6	12.5	15.7	18.7	14.82
Kinondoni	18.9	9.1	16.0	14.2	22.3	16.09
Temeke	19.8	6.2	14.8	16.8	16.3	14.78
Ubungo	20.6	4.9	16.5	17.3	22.3	16.34
Iringa	18.8	11.2	27.9	16.9	15.3	18.03
Kilimanjaro	18.9	12.5	28.9	18.6	19.9	19.74
Mara	16.8	10.5	18.1	15.6	16.4	15.47
Morogoro	13.2	4.9	10.7	18.8	15.2	12.55
Mtwara	10.4	13.4	20.3	15.9	13.5	14.69
Mwanza	15.6	12.3	21.3	15.9	21.1	17.25
Njombe	22.3	14.0	24.3	19.3	21.8	20.35
Pemba	7.2	5.7	23.3	17.6	22.3	15.21
Shinyanga	16.3	11.8	23.0	16.5	24.0	18.31
Simiyu	4.6	8.9	21.6	17.1	21.0	14.65
Tanga	16.7	10.3	21.0	19.2	23.1	18.05
Unguja	2.0	10.6	28.6	17.0	18.1	15.27
<b>Wastani</b>						<b>16.31</b>

### 1.9.4 Uwezo wa kiunganishi cha Intaneti kimataifa

Uwezo wa kuunganisha huduma ya Intaneti kwenda nje na kuja ndani ya nchi (International Internet link capacity) unawezesha ubadilishanaji wa data kati ya Tanzania na mitandao ya kimataifa, ukiwezesha upatikanaji wa maudhui ya kimataifa, huduma za wingu, na majukwaa ya mtandaoni. Kati ya uwezo uliopo, uwezo unaotumika ni asilimia 16.5. Hivyo, asilimia 83.5 ambayo ni sawa na Gbps 14,775 ipo kwa ajili ya uunganishaji mpya, kama inavyooneshwa katika Jedwali 1.9.4.1. Uwepo wa uwezo wa ziada unatoa fursa ya uwekezaji katika huduma ya intaneti ya kasi.

### Jedwali 1.9.4.1: Uwezo wa kiunganishi cha huduma ya Intaneti kufikia Machi 2026

	Uwezo unaotoka (Gbps)	Uwezo unaoingia (Gbps)
Jumla ya uwezo uliopo	17,690	17,690
Jumla ya uwezo uliotumika	2,915	2,915
Uwezo unaopatikana kwa uunganishaji	14,775	14,775

Pengo kati ya uwezo wa kiunganishi cha kimataifa uliopo na unaotumika linaonyesha fursa ya uwekezaji zaidi katika huduma za intaneti ya kasi.

### 1.9.5 Idadi ya vikoa vya intaneti

Jumla ya idadi ya vikoa vilivyosajiliwa iliongezeka kutoka 36,223 mwishoni mwa Desemba 2025 hadi 38,409 mwishoni mwa Machi 2026, kama inavyooneshwa kwenye Jedwali 1.9.5.1.

#### Jedwali 1.9.5.1: Idadi ya vikoa vya intaneti


Kikoa	Desemba 2025	Machi 2026
co.tz	28,379	30,288
or.tz	2,894	2,978
ac.tz	1,249	1,293
go.tz	947	951
.tz	2,409	2,529
sc.tz	284	302
ne.tz	25	28
me.tz	18	21
info.tz	6	6
hotel.tz	2	3
mobi.tz	3	3
tv.tz	3	3
mil.tz	4	4
<b>Jumla</b>	<b>36,223</b>	<b>38,409</b>

### 1.10 Huduma za Pesa Mtandao

Sehemu hii inawasilisha takwimu za huduma za pesa mtandao kupitia simu za mkononi zinazotolewa na watoa huduma za pesa mtandao kulingana na idadi ya akaunti za pesa mtandao na miamala

### 1.10.1 Akaunti za pesa mtandao


Idadi ya akaunti za pesa mtandao ambazo zilitumika angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita iliongezeka kwa asilimia 5.9 kutoka akaunti milioni 76.47 katika robo ya mwaka iliyoishia Desemba 2025 hadi milioni 80.98 katika robo ya mwaka iliyoishia Machi 2026 kama ilivyooneshwa katika kielelezo 1.10.1.1.



#### Jedwali 1.10.1.1: Idadi ya akaunti za pesa mtandao

	Januari	Februari	Machi
Airtel money	14,583,309	14,483,495	14,402,391
Azam Pesa	74,732	74,732	73,877
HaloPesa	7,358,608	7,748,580	7,631,532
Mpesa	31,574,589	31,689,786	33,173,927
Mixx by Yas	23,618,330	24,326,880	25,116,691
T-Pesa	536,793	566,977	578,850
<b>Jumla</b>	<b>77,746,361</b>	<b>78,890,450</b>	<b>80,977,268</b>

#### Kielelezo 1.10.1.2: Mgawanyo wa akaunti za pesa mtandao



Kielelezo 1.10.1.2 kinaonesha kuwa soko la pesa mtandao lina ushindani, ambapo Mix by Yas, Mpesa na Airtel Money zinamiliki asilimia 89 ya soko huku M-pesa ikiongoza kwa kuwa na asilimia 41.18.


### 1.10.2 Idadi ya miamala ya pesa mtandao

Mwenendo wa miamala ya pesa mtandao uliongezeka kwa asilimia 7.4 kwa robo mwaka iliyoishia Machi 2026 ikilinganishwa na robo mwaka iliyoishia Desemba 2025, kama inavyooneshwa katika Jedwali 1.10.2.1. Vilevile, idadi ya miamala iliongezeka kwa wastani wa asilimia 11 katika robo mwaka nne


**Jedwali 1.10.2.1: Idadi ya miamala ya pesa mtandao**

Kipindi	Januari	Februari	Machi
Airtel Money	130,572,078	118,053,119	137,714,126
Azam Pesa	2,431,099	2,431,099	2,845,248
HaloPesa	18,742,019	50,835,787	60,192,110
TTCL	156,537	165,522	192,345
Mpesa	249,591,512	241,780,918	308,717,427
Mixx by Yas	228,286,180	205,697,154	233,090,105
<b>Jumla</b>	<b>629,779,425</b>	<b>618,963,599</b>	<b>742,751,361</b>

**Kielelezo 1.10.2.1: Mgawanyo kiasilimia wa miamala ya pesa za simu kufikia Machi 2026 baina ya watoa huduma**



**Kielelezo 1.10.2.2: mwenendo wa Idadi ya usajili na miamala ya pesa mtandao kwa robo mwaka**



## 1.11 Ubora wa huduma (QoS)

Vipimo vya ubora wa huduma (Quality of Service - QoS) vilifanyika kwa kuzingatia vigezo vya ubora wa huduma (QoS) na mbinu za vipimo zilizoainishwa kwenye Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Ubora wa Huduma), 2025. Matokeo ya vipimo vya ubora wa huduma za mawasiliano nchini kuanzia Januari hadi Machi 2026 yanajumuisha vipengele mbalimbali kama vile upatikanaji wa mtandao, simu zilizofanikiwa kuunganishwa, simu zilizokatika na ubora wa sauti. Matokeo ya upimaji wa ubora wa huduma za simu na Intaneti kwa kipindi cha Januari hadi Machi 2025 yanaonesha kuwa Yas ilikuwa na asilimia 98.5, Vodacom ilikuwa na asilimia 98.0, Airtel ilikuwa na asilimia 92.6, TTCL ilikuwa na asilimia 91.8 na Halotel ilikuwa na asilimia 90.6 kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali 1.11.1.


**Jedwali 1.11.1: Matokeo ya ubora wa huduma za simu na Intaneti kwa robo mwaka iliyoishia Machi 2026**

Mtoa huduma	Kiwango cha ufanisi
Yas	98.5%
Vodacom	98.0%
Airtel	92.6%
TTCL	91.8%
Halotel	90.6%
<b>Wastani wa sekta</b>	<b>94.3%</b>

### 1.11.1 Upatikanaji wa mtandao

Upatikanaji wa mtandao ni kiashiria kinachoonesha upatikanaji wa mtandao wa simu wakati watumiaji wanataka kutumia huduma za mtandao huo. Lengo ni kufikia zaidi ya asilimia 99. Halotel, Yas, TTCL na Vodacom zilifikia lengo kwenye maeneo kumi na tisa kati ya maeneo kumi na tisa ambapo vipimo vilifanyika. Aidha, Airtel ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na nne kati ya maeneo kumi na tisa kama inavyooneshwa kwenye kielelezo kielelezo 1.11.1.

**Kielelezo 1.11.1.1: Upatikanaji wa Mtandao**




### 1.11.2 Simu zilizofanikiwa kuunganishwa

Simu zilizofanikiwa kuunganishwa hupimwa kwa asilimia ya simu ambazo ziliweza kuunganishwa baada ya kupiga. Lengo ni juu ya 98%.

Vodacom ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na nane kati ya maeneo kumi na tisa yaliyopimwa, Yas ilifikia lengo katika maeneo kumi na saba kati ya maeneo kumi na tisa yaliyopimwa, Halotel ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na tano, Airtel ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na tatu na TTCL ilifikia lengo kwenye maeneo nane kati ya maeneo kumi na tisa yaliyopimwa ambapo vipimo vilifanyika kama inavyooneshwa kwenye kielelezo 1.11.2.


#### Kielelezo 1.11.2.1: Simu zilizofanikiwa kuunganishwa



### 1.11.3 Simu zilizokatika

Kipimo cha kiashiria hiki ni asilimia ya simu zinazokatika kwa sababu za kiufundi kabla ya wahusika kumaliza mazungumzo yao. Lengo ni chini ya 2%. Watoa huduma wote walifikia lengo katika maeneo yote kumi na tisa ambapo vipimo vilifanyika kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.3


### Kielelezo 1.11.3.1: Matokeo ya Simu zilizokatika



### 1.11.4 Upatikanaji wa huduma ya 2G

Upatikanaji wa huduma ya 2G huonesha jinsi maeneo yaliyofikiwa na huduma hiyo na watoa huduma wa mtandao wa simu. Wateja hawawezi kupata huduma za mtandao wa simu za 2G katika maeneo ambayo hayana mtandao au yenye mtandao duni. Lengo la juu kwa teknolojia ya 2G ni -85 dBm. Airtel ilifikia lengo katika maeneo yote kumi na tisa ambapo vipimo vilifanyika, Halotel ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na nane kati ya maeneo kumi na tisa ambapo vipimo vimefanyika, Yas ilifikia lengo katika maeneo yote kumi ambapo vipimo vimefanyika, Vodacom, ilifikia lengo katika maeneo yote kumi na nne ambapo vipimo vimefanyika na TTCL ilifikia lengo katika maeneo nane kati ya maeneo kumi na moja ambapo vipimo vimefanyika kama inavyooneshwa kwenye kielelezo 1.11.4.


### Kielelezo 1.11.4.1: Matokeo linganishi kwenye upatikanaji wa huduma



### 1.11.5 Upatikanaji wa huduma ya 3G

Upatikanaji wa huduma ya 3G huonesha jinsi maeneo yaliyofikiwa na huduma hiyo na watoa huduma wa mtandao wa simu. Wateja hawawezi kupata huduma za mtandao wa simu za 3G katika maeneo ambayo hayana mtandao au yenye mtandao duni. Lengo la juu kwa teknolojia ya 3G ni -95 dBm. Watoa huduma wote walifikia lengo katika maeneo yote kumi na tisa ambapo vipimo vimefanyika kama inavyooneshwa kwenye kielelezo 1.11.5.


**Kielelezo 1.11.5.1: Matokeo ya kulinganisha upatikanaji wa huduma ya 3G**



### 1.11.6 Upatikanaji wa huduma ya 4G

Upatikanaji wa huduma ya 4G huonesha jinsi maeneo yaliyofikiwa na huduma hiyo na watoa huduma wa mtandao wa simu. Lengo la juu kwa teknolojia ya 4G ni -100 dBm. Airtel, Yas na TTCL walifikia lengo katika maeneo kumi na tisa ambapo vipimo vilifanyika. Aidha, Halotel na Vodacom zilifikia lengo katika maeneo kumi na nane kati ya kumi na tisa ambapo vipimo vimefanyika kama inavyooneshwa kwenye kielelezo 1.11.6.


### Kielelezo 1.11.6.1: Matokeo linganishi kwenye upatikanaji wa huduma ya 4G



### 1.11.7 Kasi ya data

Kasi ya kupakua data ni kipimo cha kasi ya uhamishaji data kwenye mtandao. Hupima jinsi data inavyohamishwa haraka kutoka kwa itifaki (protocol) ya uhamishaji faili (File Transfer Protocol - FTP) hadi kwa kifaa cha mawasiliano ya simu. Lengo ni wastani kuwa sawa au zaidi ya 10,000 Kbps. Yas, TTCL na Vodacom zilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na nane ambapo vipimo vilifanyika. Airtel zilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na tano kati ya kumi na nane yaliyopimwa na Halotel alifikia lengo katika maeneo tisa kati ya kumi nane yaliyopimwa kama inavyooneshwa kwenye kielelezo 1.11.7.


### Kielelezo 1.11.7.1: Matokeo linganishi kwenye kasi ya data



### 1.11.8 Muda wa kupata huduma ya data

Muda wa kupata huduma ya data hupimwa kwa muda ambao kifaa cha mtumiaji huchukua kutuma ombi na kupokea jibu kutoka kwenye seva. Lengo ni wastani kuwa chini ya 200ms. Watoa huduma wote walifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na tisa yaliyopimwa kama inavyooneshwa kwenye kielelezo 1.11.8.


**Kielelezo 1.11.8: Matokeo linganishi ya muda wa kupata huduma ya data**



### 1.11.9 Muda wa kufika ujumbe mfupi wa maneno (SMS)

Muda wa kufika ujumbe mfupi wa maneno (SMS) inapima muda unaotumika kutoka ujumbe mfupi wa maneno (SMS) inavyotumwa mpaka inapofika kwenye simu husika. Lengo ni chini ya sekunde 2. Yas, Halotel na Vodacom zilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na nane ambapo vipimo vilifanyika. Watoa huduma wote walifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na tisa yaliyopimwa kama inavyooneshwa kwenye kielelezo 1.11.9.


**Kielelezo 1.11.9.1: Matokeo ya muda wa kufika ujumbe**



### 1.11.10 Muda wa kuanzisha simu

Muda wa kuanzisha simu hupimwa kwa muda ambao simu inachukua kuunganishwa baada ya kupiga. Lengo ni chini ya sekunde 8. Airtel, Halotel, Yas na Vodacom walifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na tisa yaliyopimwa. Aidha, TTCL ilifikia lengo katika maeneo kumi nane kati ya kumi na tisa yaliyopimwa kama inavyooneshwa kwenye kielelezo kama inavyooneshwa kwenye kielelezo 1.11.10..


**Kielelezo 1.11.10.1: Matokeo ya kulinganisha muda wa kuanzisha simu**



### 1.11.11 Ubora wa sauti

Ubora wa Sauti ni kipimo cha utambuzi wa ubora wa sauti wakati wa mazungumzo ya simu. Kiwango cha alama ya ubora wa sauti ni kati ya 1 hadi 5, huku 1 ikiwa duni na 5 ikiwa ni ubora mzuri wa sauti. Lengo ni wastani wa sampuli zote za vipimo vya ubora wa sauti kuwa zaidi ya 4. Airtel, Yas na TTCL zilifikia lengo katika maeneo kumi na tatu kati ya maeneo kumi na nne ambapo vipimo vilifanyika, wakati Halotel ilifikia lengo kwenye maeneo tisa kati ya maeneo kumi nne na Vodacom ilifikia lengo kwenye maeneo tisa katika ya kumi na mbili ambapo vipimo vimefanyika kama inavyooneshwa kwenye kielelezo 1.11.11.


**Kielelezo 1.11.11.1: Matokeo ya ubora wa sauti**



### 1.12 Majaribio ya ulaghai

Takwimu zinaonesha, idadi ya majaribio ya ulaghai yaliongezeka kwa asilimia 3.9 kutoka majaribio 9,450 yalioripotiwa robo mwaka iliyoishia Desemba 2025 na kufikia majaribio 9,816 katika robo mwaka iliyoishia Machi 2026 kama ilivyooneshwa katika Jedwali 1.12.1. Wakati TTCL ikiongoza kwa kuwa na majaribio mengi zaidi ya ulaghai ikilinganishwa na watoa huduma wengine, takwimu zinaonesha mwenendo tofauti wa majaribio ya ulaghai kwa kila mtoa huduma. TTCL iliongozwa kwa kuwa na mgawanyo mkubwa wa majaribio ya ulaghai kwa watoa huduma wote kama inavyooneshwa kwenye Kielelezo 1.12.1. Jedwali 1.12.2 linaonesha idadi ya majaribio ya ulaghai kimkoa kwa robo mwaka inayoishia Machi 2026.

**Kielelezo 1.12.1: Mgawanyo wa asilimia ya majaribio ya ulaghai mtandaoni kwa kila mtoa huduma kwa robo mwaka inayoishia Machi 2026**



**Table 1.12.1 Majaribio ya ulaghai kwa kila mtoa huduma**

Robo ya mwaka	Airtel	Halotel	Yas	TTCL	Vodacom	Total
Machi 2026	1,399	500	2,659	3,375	1,883	9,816
Desemba 2025	1,174	1,149	2,257	2,225	2,645	9,450
<b>Badiliko</b>	19.2%	-56.5%	17.8%	51.7%	-28.8%	3.9%


## Jedwali 1.12.2: Idadi ya Majaribio ya ulaghai kwa mkoa

Tanzania bara						
Mkoa	Airtel	Halotel	Yas	TTCL	Vodacom	Jumla
Rukwa	128	134	216	3,027	440	3,945
Morogoro	313	108	1,387	6	786	2,600
Dar es salaam	516	63	185	27	128	919
Mbeya	31	34	102	33	113	313
Arusha	47	5	44	8	115	219
Katavi	-	13	10	151	24	198
Kilimanjaro	22		51	2	108	183
Mwanza	62	3	42	10	11	128
Pwani	25	18	58	7	11	119
Manyara	13	28	40	11	22	114
Dodoma	24	16	57	2	10	109
Mara	13	1	30	4	56	104
Songwe	29	22	32	11		94
Tanga	16	7	57	5	5	90
Njombe	4	9	57	1	4	75
Tabora	24	9	25	14	2	74
Geita	28	2	25	7	5	67
Kagera	17	1	39		9	66
Iringa	10	11	19	5	5	50
Shinyanga	11		18	8	9	46
Singida	8	1	25	7	5	46
Ruvuma	4	3	27	3	6	43
Simiyu	10	3	20	8	1	42
Mtwara	12	2	21	5		40
Mjini	9	2	27		1	39
Magharibi						
Kigoma	8	2	15	9	2	36
Lindi	7	3	16	3	1	30
Zanzibar						
Kusini Unguja	-	-	5	-	-	5
Kusini Pemba	-	-	3	1	-	4
Kaskazini Pemba	-	-	3	-	-	3
Kaskazini Unguja	-	-	3	-	-	3
<b>Jumla</b>	<b>1,399</b>	<b>500</b>	<b>2,659</b>	<b>3,375</b>	<b>1,883</b>	<b>9,816</b>

Kielelezo 1.12.2 kinaonesha mgawanyo wa majaribio ya ulaghai kimkoa, ambapo Rukwa na Morogoro zilikuwa na idadi kubwa zaidi ya majaribio ya ulaghai.

### Kielelezo 1.12.2: Idadi majaribio ya ulaghai kimkoa kwa robo mwaka inayoishia Machi 2026

#### Tanzania Bara



#### Zanzibar



### Jedwali 1.12.3: Majaribio ya ulaghai kiwilaya kwa mikoa minne inayoongoza

Mkoa	Wilaya	Majaribio ya ulaghai
Rukwa	Sumbawanga	1,830
	Kalambo	1,136
	Nkasi	979
Morogoro	Kilombero	2,297
	Ulanga	124
	Malinyi	58
	Kilosa	54
	Morogoro	40
	Mvomero	19
	Gairo	8
Dar es Salaam	Ubungo	295
	Ilala	232
	Temeke	193
	Kinondoni	192
	Kigamboni	27
Mbeya	Mbeya	155
	Mbozi	52
	Rungwe	42
	Mbarali	32
	Chunya	22

### 1.13. Leseni za huduma ya Mawasiliano ya simu na intaneti

Mpaka kufikia Machi 2026, kulikuwa na leseni hai 1,816 kwenye sekta ndogo ya mawasiliano ya simu na intaneti kama inavyooneshwa kwenye jedwali 1.13.1

**Jedwali 1.13.1. Leseni za huduma ya Mawasiliano ya simu na intaneti**

Aina ya leseni	Idadi ya leseni	
	Desemba 2025	Machi 2026
Leseni za Miundombinu ya Mawasiliano	48	52
Leseni za utumiaji wa Miundombinu ya mtandao	24	25
Leseni za matumizi ya huduma	159	173
Vituo vya Ndege	194	192
Vituo vya Amatuer	17	19
Vituo vya VSAT vya Kudumu	21	18
Vituo vya VSAT vya kuhamishika	-	-
Vituo vya Ardhini vya Satelaiti	-	-
Vituo vya Meli	42	43
Vituo vya Redio vya HF	16	18
Virejeshi vya Mawimbi vya Redio vya VHF-UHF		
Vituo vya Redio vya VHF-UHF vyenye Jozi ya Masafa	125	126
Vituo vya Redio vya VHF-UHF vyenye Masafa Moja	184	179
Ufungaji na Matengenezo	225	241
Usambazaji wa Kitaifa (Wauzaji wa Jumla)	63	61
Uingizaji wa Kitaifa	178	182
Utoaji wa Namba	515	527

## 1.14. Vyeti

Mpaka kufikia Machi 2026, vyeti 5,970 vilitolewa kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali 1.14.1

### Jedwali 1.14.1 Vyeti

Aina ya cheti	Idadi ya vyeti	
	Desemba 2025	Machi 2026
Mfumo wa Kimataifa wa Tahadhari na Usalama wa Baharini	316	381
Uidhinishaji wa vifaa vya mawasiliano	5,538	5,538
Usajili wa Simu za Mkononi za Satelaiti	51	51

Viambatisho vya Majedwali ya takwimu za  
Huduma za mawasiliano ya simu na intaneti

### Jedwali 1: Mwenendo wa idadi ya Usajili wa Huduma za Mawasiliano ya Simu

Kwa robo mwaka					
	Juni 2025	Septemba 2025	Desemba 2025	Machi 2026	
Miundombinu inayohamishika	92,656,179	99,184,621	106,823,601	111,795,302	
Miundombinu isiyohamishika	79,619	111,169	111,600	111,933	
Jumla	92,735,798	99,295,790	106,935,201	111,907,235	
Upenyo	136.1%	145.7%	156.9%	159.8%	
Kwa mwaka					
	2021	2022	2023	2024	2025
Miundombinu inayohamishika	54,044,384	60,192,331	70,215,144	86,769,161	106,823,601
Miundombinu isiyohamishika	71,834	84,696	75,732	78,299	111,600
Jumla	54,118,218	60,277,027	70,290,876	86,847,460	106,935,201
Upenyo	88.0%	98.0%	111.0%	133.5%	156.9%

### Jedwali 2: Mwenendo wa wastani wa bei za huduma ya mawasiliano ya simu (TZS) kwa robo mwaka

Ndani ya nchi					
	Juni 2025	Septemba 2025	Desemba 2025	Machi 2026	
Ndani ya mtandao	26.00	29.00	29.00	29.00	
Nje ya mtandao	28.00	29.00	29.00	29.00	
	2021	2022	2023	2024	2025
Ndani ya mtandao	34.00	32.00	29.00	26.00	27.50
Nje ya mtandao	34.00	32.00	30.00	28.00	28.50
Nje ya nchi					
	Juni 2025	Septemba 2025	Desemba 2025	Machi 2026	
EA	247.52	247.52	247.52	247.52	
RoW	2,175.15	2,315.82	2,315.82	2,315.82	
	2021	2022	2023	2024	2025
EA	966.00	1,103.00	1,171.00	684.00	342.59
RoW	1,564.00	1,817.00	1,776.00	2,055.00	2,185.45

### Jedwali 3: Mwenendo wa wastani wa bei za huduma za SMS za nje ya kifurushi (TZS)

Kwa robo mwaka					
	Juni 2025	Septemba 2025	Desemba 2025	Machi 2026	
SMS Kitaifa	7.80	8.10	8.10	7.80	
SMS Kimataifa	189.60	189.60	189.60	189.60	
Mwaka					
	2021	2022	2023	2024	2025
SMS Kitaifa	13.00	11.00	11.00	7.80	7.95
SMS Kimataifa	172.00	193.00	200.00	189.60	189.60

### Jedwali 4: Mwenendo wa wastani wa bei za huduma za SMS za ndani ya kifurushi (TZS)

Kwa robo mwaka					
	Juni 2025	Septemba 2025	Decemba 2025	Machi 2025	
Ndani ya mtandao	4.80	5.48	5.11	4.80	
Nje ya mtandao	5.96	6.24	6.33	6.07	
SMS	1.52	1.46	1.44	1.55	
Data	2.12	2.08	2.06	2.12	
Kwa mwaka					
	2021	2022	2023	2024	2025
Ndani ya mtandao	7.84	7.27	4.90	4.68	5.05
Nje ya mtandao	8.69	7.78	6.30	6.22	6.15
SMS	3.35	2.69	1.37	1.46	1.49
Data	1.61	1.86	2.14	2.17	2.10

**Jedwali 5: Mwenendo wa idadi ya dakika za huduma ya mawasiliano ya simu ndani na nje ya mtandao**

Kwa robo mwaka					
	Juni 2025	Septemba 2025	Desemba 2025	Machi 2026	
Ndani ya mtandao	21,492,956,952	23,574,844,856	24,703,982,204	22,950,337,624	
Nje ya mtandao	21,759,205,362	23,776,107,671	22,514,227,953	22,490,621,092	
<b>Jumla</b>	<b>43,252,162,314</b>	<b>47,350,952,527</b>	<b>47,218,210,157</b>	<b>45,440,958,716</b>	
Kwa mwaka					
	2021	2022	2023	2024	2025
Ndani ya mtandao	51,673,651,476	62,678,814,642	77,770,241,513	81,916,822,649	89,994,948,074
Nje ya mtandao	43,194,917,029	60,064,367,493	67,100,445,506	76,215,903,038	88,394,850,674
<b>Jumla</b>	<b>94,868,568,505</b>	<b>122,743,182,135</b>	<b>144,870,687,019</b>	<b>158,132,725,687</b>	<b>178,389,798,748</b>

**Jedwali 6: Mwenendo wa idadi ya dakika za huduma ya mawasiliano ya simu kutoka na kwenda Afrika Mashariki (EA), Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) na Mtaifa mengine (RoW)**

Kwa robo mwaka					
	Juni 2025	Septemba 2025	Desemba 2025	Machi 2026	
Kwenda EA	156,913,941	143,487,145	147,904,598	157,378,250	
Kutoka EA	34,761,058	39,343,813	42,845,139	42,566,883	
Kwenda SADC	310,606	270,090	411,946	279,353	
Kutoka SADC	835,650	618,503	908,220	533,936	
kwenda RoW	2,224,864	2,410,516	5,198,076	2,157,787	
Kutoka RoW	4,155,135	3,466,597	6,813,551	4,360,996	
Kwa mwaka					
	2021	2022	2023	2024	2025
Kwenda EA	9,097,165	8,927,113	95,473,684	363,293,881	577,704,620
Kutoka EA	15,853,362	13,594,473	34,994,641	108,663,455	147,959,242
Kwenda RoW	24,856,947	26,034,131	19,510,999	36,294,294	14,823,361
Kutoka RoW	49,885,142	33,374,619	23,681,940	24,858,074	22,412,244

## Jedwali 7: Idadi ya SMS

Kwa robo mwaka				
	Juni 2025	Septemba 2025	Desemba 2025	Machi 2026
Ndani ya mtandao	22,301,400,244	22,288,636,639	24,195,043,702	91,398,139,909
Nje ya mtandao	30,516,070,406	30,654,884,978	33,609,424,008	127,250,784,021
<b>Jumla</b>	<b>52,817,470,650</b>	<b>52,943,521,617</b>	<b>57,804,467,710</b>	218,648,923,930

Kwa mwaka					
	2021	2022	2023	2024	2025
Ndani ya mtandao	58,875,779,663	65,358,270,089	84,818,793,761	84,909,556,665	89,866,764,116
Nje ya mtandao	78,200,512,436	88,154,239,625	121,727,776,013	116,828,465,147	123,717,687,842
<b>Jumla</b>	<b>137,076,292,099</b>	<b>153,512,509,714</b>	<b>206,546,569,774</b>	<b>201,738,021,812</b>	<b>213,584,451,958</b>

## Jedwali 8: Idadi ya SMS Kutoka na kwenda EA, SADC and RoW

Kwa robo mwaka				
	Juni 2025	Septemba 2025	Decemba2025	March 2026
Kwenda EA	427,754	461,683	388,998	57,273.0
Kutoka EA	10,495,680	11,533,796	601,520	149,752.0
Kwenda SADC	85,843	102,830	142,093	18,126.0
Kutoka SADC	952,425	902,391	407,450	112,001.0
kwenda RoW	1,128,292	1,334,976	1,518,656	405,079.0
Kutoka RoW	2,118,318,349	2,667,331,794	2,033,965	140,348.0

Kwa mwaka					
	2021	2022	2023	2024	2025
Kwenda EA	1,425,624	1,700,525	2,233,288	1,896,295	1,714,111
Kutoka EA	89,717,530	58,344,672	37,592,410	41,662,728	30,466,692
Kwenda RoW	3,191,041	3,574,956	5,448,764	13,342,306	5,658,259
Kutoka RoW	4,599,468,894	4,664,200,079	5,562,047,440	5,798,188,788	6,576,719,572

## Jedwali 9: Mwenendo wa idadi ya usajili kwa kipindi cha miaka mitano

	2021	2022	2023	2024	2025
Idadi ya usajili	29,103,482	31,172,544	35,885,592	48,028,227	58,106,264

### Jedwali 10: Matokea ya kipimo cha kasi ya upakuaji kwa kila mtoa huduma kwa maeneo yaliyopimwa kwa robo mwaka inayoishia Machi 2026

Eneo lililopimwa	Airtel	Halotel	Yas	TTCL	Vodacom	Wastani
Arusha	24.3	17.7	32.7	27.3	33.8	27.18
Ilala	40.1	17.0	50.3	26.2	51.8	37.07
Kigamboni	31.0	15.2	39.3	19.3	41.6	29.26
Temeke	40.0	18.6	55.6	23.8	24.8	32.54
Kinondoni	39.3	21.8	67.2	16.2	52.4	39.38
Ubungo	35.6	18.8	53.8	19.9	48.3	35.30
Geita	34.8	23.7	33.8	26.6	47.3	33.24
Kagera	32.0	25.0	30.5	31.0	40.4	31.79
Kigoma	25.2	21.2	32.7	22.5	20.2	24.38
Kilimanjaro	24.6	18.9	51.6	25.4	26.6	29.44
Manyara	22.8	19.3	42.2	22.4	24.2	26.17
Mbeya	20.2	-	34.5	-	47.1	33.95
Pwani	29.6	22.4	40.4	24.0	22.3	27.72
Rukwa	26.5	22.7	33.4	24.5	16.7	24.76
Singida	22.7	21.1	44.2	26.2	27.4	28.32
Songwe	27.6	-	40.5	-	36.6	34.89
Tabora	23.9	22.9	38.6	24.2	21.4	26.21
Unguja	13.4	14.9	40.2	23.4	27.5	23.88
<b>Wastani</b>						<b>30.30</b>

### Jedwali 11: Matokea ya kipimo cha kasi ya ukawiaji kwa kila mtoa huduma kwa maeneo yaliyopimwa kwa robo mwaka inayoishia Machi 2026

Eneo lililopimwa	Airtel	Halotel	Yas	TTCL	Vodacom	Wastani
Arusha	41.9	64.9	94.0	110.7	50.6	72.40
Ilala	39.2	57.4	70.4	96.7	35.7	59.85
Kigamboni	44.7	50.7	78.5	106.4	41.1	64.28
Temeke	41.9	68.5	74.9	102.6	42.8	66.12
Kinondoni	49.7	46.5	67.4	119.5	36.1	63.83
Ubungo	53.4	57.3	75.4	101.0	39.8	65.39
Geita	92.7	48.7	135.7	129.8	65.5	94.45
Kagera	59.9	55.3	113.8	116.7	52.7	79.64
Kigoma	71.6	68.5	142.9	151.4	60.3	98.93
Kilimanjaro	36.9	63.7	63.8	101.7	50.8	63.38
Manyara	49.1	47.0	92.9	105.3	50.4	68.94
Mbeya	62.9	-	97.5	-	48.0	69.47
Pwani	44.1	43.6	70.0	97.6	42.6	59.58
Rukwa	70.5	69.4	134.5	119.1	67.1	92.10
Singida	55.0	64.1	93.4	110.5	48.0	74.17
Songwe	58.3	-	92.7	-	48.2	66.42
Tabora	60.7	61.2	112.3	123.3	56.2	82.76
Unguja	72.0	70.1	43.8	96.5	53.0	67.07
<b>Wastani</b>						<b>72.71</b>

## Jedwali 12: Matokeo ya kipimo cha upatikanaji wa huduma kwa kila mtoa huduma kwa maeneo yaliyopimwa kwa robo mwaka inayoishia Machi 2026

Eneo lililopimwa	Airtel	Halotel	Yas	TTCL	Vodacom	Wastani
Arusha	98.9	99.1	100.0	99.8	99.3	99.43
Ilala	100.0	100.0	100.0	100.0	100.0	100.00
Kigamboni	100.0	100.0	99.9	100.0	99.6	99.89
Kinondoni	99.5	99.9	99.9	99.9	99.7	99.78
Temeke	99.8	99.5	100.0	99.8	99.6	99.73
Ubungo	100.0	99.5	99.7	99.8	99.2	99.64
Iringa	100.0	100.0	100.0	100.0	99.5	99.89
Kilimanjaro	100.0	99.5	99.9	99.8	100.0	99.82
Mara	98.5	99.7	100.0	100.0	99.4	99.53
Mbeya	100.0	100.0	99.7	99.8	99.6	99.82
Morogoro	100.0	100.0	100.0	99.9	100.0	99.97
Mtwara	99.9	100.0	100.0	100.0	100.0	99.97
Mwanza	98.5	99.5	100.0	100.0	100.0	99.60
Njombe	98.2	100.0	100.0	100.0	99.8	99.59
Pemba	100.0	100.0	100.0	100.0	100.0	100.00
Shinyanga	99.6	99.8	99.9	99.9	99.4	99.72
Simiyu	98.5	99.7	100.0	99.9	99.1	99.43
Tanga	99.4	99.6	99.9	100.0	99.9	99.76
Unguja	100.0	100.0	100.0	100.0	100.0	100.00
<b>Wastani</b>						<b>99.77</b>

## Jedwali 13: Huduma za Pesa Mtandao

	Kwa mwaka				
	2021	2022	2023	2024	2025
<b>Idadi ya akaunti za pesa mtandao</b>	35,285,767	40,953,496	52,875,129	63,207,569	76,466,691
<b>Idadi ya miamala ya kifedha</b>	3,752,084,894	4,195,899,414	5,273,086,154	3,737,202,434	6,306,767,827
	Kwa robo mwaka				
	Juni 2025	Septemba 2025	Desemba 2025	Machi 2026	
<b>Idadi ya akaunti za</b>	68,059,290	72,497,350	76,466,691	80,977,268	
<b>Idadi ya miamala ya kifedha</b>	1,392,683,175	1,694,032,906	1,853,717,380	1,991,494,385	

Sura ya pili 02

# Huduma za Utangazaji



# Huduma za Utangazaji

Sura hii inawasilisha takwimu katika huduma ya utangazaji, ikijumuisha huduma za televisheni kwa njia ya mitambo iliyosimikwa ardhini (DTT), setelaiti (DTH), na kwa njia ya waya (Cable TV), ueneaji wa mtandao na utekelezaji wa masharti ya leseni. Kwa ujumla, takwimu hizo zinacoeleza muundo, ufikaji na utendaji wa sekta ya utangazaji. Katika kipindi cha marejeo, visimbuzi milioni 2.09 vililipiwa, na televisheni 17,803 ziliunganishwa kwa njia ya waya

## 2.1. Visimbuzi Vilivyolipiwa

Idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa kwa ajili ya kupata huduma za utangazaji za televisheni ilipungua kwa asilimia 1, katika kipindi cha marejeo, kama ilivyooneshwa kwenye kielelezo hapo chini. Kielelezo 2.1.1 kinaonesha kuwa visimbuzi vilivyounganishwa kwa njia ya satelaiti (DTH) vilikua ni vingi ikilinganishwa na visimbuzi vilivyounganishwa kwa njia ya mitambo iliyosimikwa ardhini (DTT). DTH zilichangia asilimia 75.2 ya jumla visimbuzi vilivyolipiwa, wakati DTT zilichangia asilimia 24.8.

Kufikia Desemba 2025

**Milioni 2.11**


Kufikia Machi 2026

**Milioni 2.09**

**1%**




Kielelezo 2.1.1: Mgawanyiko wa visimbuzi vilivyolipiwa



Vilevile, kati ya watoa huduma watano, Azam Media Limited ilikuwa na idadi kubwa ya visimbuzi vilivyolipiwa sawa sawa na asilimia 71.1, ikifuatiwa na Star Media Limited ikiwa na asilimia 16.3, kama inavyooneshwa kwenye Kielelezo 2.1.2.

**Kielelezo 2.1.2: Idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa kwa robo mwaka inayoishia Machi 2026**




**Jedwali 2.1.1: Idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa kwa kila mtoa huduma kwa robo mwaka inayoishia Machi 2026**

Mtoa huduma	DTT	DTH	Jumla
Azam Media Limited	327,734	1,160,235	1,487,969
Basic Transmissions Limited (Continental)	32,663	27,349	60,012
Multichoice Tanzania Limited (DStv)	-	189,651	189,651
Star Media Limited	157,981	183,546	341,527
Zuku	N/A	12,885	12,885
<b>Jumla</b>	<b>518,378</b>	<b>1,573,666</b>	<b>2,092,044</b>

Mgawanyo wa visimbuzi vilivyolipiwa kwa kila mkoa, unaashiria kwamba idadi kubwa ya visimbuzi vilivyolipiwa vipo kwenye miji mikubwa, kama inavyooneshwa katika Kielelezo 2.1.3. Miji ya Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, na Arusha, ilichangia asilimia 52.9 ya visimbuzi vyote katika kipindi cha marejeo. Wakati utofauti kwenye mgawanyo unaonesha uwepo mkubwa wa huduma za utangazaji kwenye maeneo yenye watu wengi na yenye shughuli nyingi za kibiashara, pia unaonesha maeneo yenye fursa za ukuaji.

## Ramani 2.1: Idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa vifurushi kwa kila mkoa




## 2.2. Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya

Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya (Cable TV subscriptions) iliongezeka kwa asilimia 3 kutoka 17,280 kwa robo mwaka inayoishia Desemba 2025 na kufikia 17,803 kwa robo mwaka inayoishia Machi 2026, kama inavyooneshwa kwenye Kielelezo 2.2.1. Mgawanyo wa televisheni kwa njia ya waya kwa kila mkoa unaonesha kuwa asilimia 59.2 ya televisheni zote zimeenea zaidi maeneo ya Shinyanga, Dar es Salaam, Tabora na Mwanza kama inavyooneshwa katika Kielelezo 2.2.2. Kwa ujumla, kuna utumiaji tofauti wa televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya kwenye mikoa, utofauti huo unatokana na mapendeleo ya watumiaji pamoja na uwepo wa majukwaa mbadala yanayotoa huduma ya utangazaji.

**Kielelezo 2.2.2: Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia**



**Kielelezo 2.2.2: Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya kimkoa**



Mwenendo wa idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya kwa robo mwaka na kipindi cha miaka mitano imeoneshwa kwenye jedwali 2.2.1 na 2.2.2

**Jedwali 2.2.1:** Mwenendo wa idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya kwa robo mwaka

	Juni 2025	Septemba 2025	Desemba 2025	Machi 2026
Idadi ya usajili	17,657	16,957	17,280	17,803

**Jedwali 2.2.2:** Mwenendo wa idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya kwa kipindi cha miaka mitano

	2021	2022	2023	2024	2025
idadi ya usajili	17,657	16,957	17,280	16,767	17,280

### 2.3. Ueneaji wa huduma za utangazaji

Ueneaji wa huduma za utangazaji iliyoonyeshwa katika Jedwali 2.3.1 unaonesha tofauti kubwa kati ya teknolojia za utangazaji za DTT, DTH, na FM. Kijiografia DTH imeenea kikamilifu na kwa idadi kubwa ya watu, ikitumika kama miundombinu muhimu kwa kufikia maeneo ya mbali

**Jedwali 2.3.1:** Ueneaji wa huduma za utangazaji hadi kufikia Machi 2026

Kiashiria	Desemba 2025	Machi 2026
% ya watu waliofikiwa na mawimbi na DTT	58.00%	58.00%
% ya watu waliofikiwa mawimbi na DTH	100.00%	100.00%
% ya watu waliofikiwa na mawimbi ya redio za FM	83.94%	85.31%
% ya eneo lililofikiwa mawimbi na DTT	33.00%	33.00%
% ya eneo lililofikiwa mawimbi na DTH	100.00%	100.00%
% ya eneo lililofikiwa na mawimbi redio za FM	59.15%	62.19%

### 2.4. Utekelezaji wa masharti ya leseni za utangazaji

Ufuatiliaji wa maudhui kwa watoa huduma za utangazaji wa kitaifa nchini (Televisheni na Redio) ulifanyika kuanzia Januari hadi Machi 2026 kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Ubora wa Huduma), 2025. Ili kufanikisha hili, watoa huduma za utangazaji wa kitaifa wanatakiwa kuwasilisha ratiba ya vipindi (muda, mpango, na idadi) na kuzingatia ratiba ya vipindi waliyoitoa.

### 2.4.1. Uwasilishaji na uzingatiaji wa ratiba ya vipindi

Katika kipindi cha marejeo, asilimia 63 ya chaneli za televisheni zilikidhi matakwa ya kuwasilisha ratiba ya vipindi. Ingawa, asilimia 44 pekee walizingatia ratiba walizowasilisha, kama inavyooneshwa katika Jedwali 2.4.1.1. Kwa upande mwingine, asilimia 75 ya stesheni za Radio zilikidhi matakwa ya kuwasilisha ratiba ya vipindi, na asilimia 75 zilizingatia ratiba walizowasilisha, kama inavyooneshwa katika Jedwali 2.4.1.2.

**Jedwali 2.4.1.1: Uwasilishaji na uzingatiaji wa mpango wa vipindi vya televisheni kwa robo mwaka iliyoishia Machi 2026**

Jina la televisheni	Uwasilishaji wa ratiba ya vipindi	Uzingatiaji wa ratiba ya vipindi
ITV	Imekidhi	Imekidhi
UTV	Imekidhi	Haijakidhi
Tumaini TV	Imekidhi	Imekidhi
Channel Ten Television	Haijakidhi	Haijakidhi
East Africa TV	Imekidhi	Imekidhi
Star TV Tanzania	Haijakidhi	Haijakidhi
TBC 1	Imekidhi	Imekidhi
TV Imaan	Imekidhi	Imekidhi
Arise and Shine TV	Imekidhi	Haijakidhi
WRM TV	Haijakidhi	Haijakidhi
Clouds TV	Imekidhi	Imekidhi
Hope Channel Tanzania	Imekidhi	Imekidhi
Upendo TV	Imekidhi	Haijakidhi
Mahaasin TV	Imekidhi	Haijakidhi
Channel Ten Plus	Haijakidhi	Haijakidhi
TVE	Haijakidhi	Haijakidhi

### Jedwali 2.4.1.2: Uwasilishaji na uzingatiaji wa mpango wa vipindi vya redio kwa robo mwaka iliyoishia Machi 2026

Jina la redio	Uwasilishaji wa ratiba ya vipindi	Uzingatiaji wa ratiba ya vipindi
Radio One	Imekidhi	Imekidhi
TBC Taifa	Imekidhi	Imekidhi
Adventist World Radio (AWR)	Imekidhi	Imekidhi
Clouds FM	Haijakidhi	Haijakidhi
East Africa Radio	Imekidhi	Imekidhi
EFM	Imekidhi	Imekidhi
Wasafi FM	Haijakidhi	Haijakidhi
Magic FM	Haijakidhi	Haijakidhi
TBC International	Imekidhi	Imekidhi
Radio Free Africa	Imekidhi	Imekidhi
Bongo FM	Imekidhi	Imekidhi

#### 2.4.2. Uanuai wa vipindi, maudhui ya elimu na uzingatiaji wa uwasilishaji wa habari

Watoa huduma za utangazaji wenye leseni za kitaifa (national broadcasters) wanatakiwa kurusha aina mbalimbali za maudhui yanayohakikisha utofauti wa taarifa, elimu, na vipindi vya burudani, ili kukidhi ladha, tamaduni, na maslahi tofauti ya hadhira ya Watanzania.

Katika kipindi husika, asilimia 81 ya vituo vya televisheni vilionesha utofauti mkubwa wa vipindi, na vingi vilizingatia sharti la kurusha dakika 90 za vipindi vya habari na maudhui ya elimu, kama inavyoonekana katika Jedwali 2.4.2.1. Asilimia 92 ya vituo vyote vya redio vilifikia utii kamili katika utofauti wa vipindi na maudhui ya elimu na vilifuata sharti la kurusha dakika 90 za vipindi vya habari, kama inavyooneshwa katika Jedwali 2.4.2.2.

#### Jedwali 2.4.2.1: Uanuai wa vipindi vya televisheni kwa robo mwaka iliyoishia Machi 2026

Jina la Televisheni	Utofauti wa vipindi	Maudhui ya elimu	Uzingatiaji wa dakika tisini wa habari
ITV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
UTV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Tumaini TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Channel Ten Television	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
East Africa TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Star TV Tanzania	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
TBC 1	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
TV Imaan	Imekidhi	Imekidhi	Haijakidhi
Arise and Shine TV	Haijakidhi	Haijakidhi	Haijakidhi
WRM TV	Haijakidhi	Haijakidhi	Imekidhi
Clouds TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Hope Channel Tanzania	Imekidhi	Imekidhi	Haijakidhi
Upendo TV	Imekidhi	Imekidhi	Haijakidhi
Mahaasin TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Channel Ten Plus	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi

#### Jedwali 2.4.2.2: Uanuai wa vipindi vya redio kwa robo mwaka iliyoishia Machi 2026

Jina la redio	Utofauti wa vipindi	Maudhui ya elimu	Uzingatiaji wa dakika tisini wa habari
Radio One	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
TBC Taifa	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Adventist World Radio (AWR)	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Clouds FM	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
East Africa Radio	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
EFM	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Wasafi FM	Haijakidhi	Haijakidhi	Haijakidhi
Magic FM	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
TBC International	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Radio Free Africa	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Bongo FM	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Radio Maria	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi

### 2.4.3. Uzingatiaji wa maudhui ya ndani (local content)

Watoa huduma za utangazaji wenye leseni za kitaifa (national broadcasters) wanatakiwa kuhakikisha kwamba asilimia 60 ya vipindi vya vimevengenezwa ndani ya nchi, ili kuchagiza utamaduni, lugha, na maudhui ya ndani ya nchi. Katika kipindi cha marejeo, chaneli za televisheni zilikidhi takwa hilo kama inavyooneshwa katika Jedwali 2.4.3.1. Stesheni za redio zilikidhi kwa kuzingatia takwa la utoaji wa maudhui ya ndani kama inavyooneshwa katika Jedwali 2.4.3.2.

#### Jedwali 2.4.3.1: Uzingatiaji wa maudhui ya ndani kwenye vipindi vya televisheni kwa robo mwaka iliyoishia Machi 2026

Jina la Televisheni	Yenye manufaa kwa jamii	Lugha (Kiswahili au Kingereza)	60% ya uzalishaji wa maudhui ya ndani	80% Muziki wa kitanzania
TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
UTV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Tumaini TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Channel Ten Television	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
East Africa TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Star TV Tanzania	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
TBC 1	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
TV Imaan	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Arise and Shine TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
WRM TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Clouds TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Hope Channel Tanzania	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Upendo TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Mahaasin TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Channel Ten Plus	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
TVE	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi

### Jedwali 2.4.3.2: Uzingatiaji wa maudhui ya ndani kwenye vipindi vya redio kwa robo mwaka iliyoishia Machi 2026

Jina la redio	Yenye manufaa kwa jamii	Lugha (Kiswahili au Kingereza)	60% ya uzalishaji wa maudhui ya ndani	80% Muziki wa kitanzania
Radio One	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
TBC Taifa	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Adventist World Radio (AWR)	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Clouds FM	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
East Africa Radio	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
EFM	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Wasafi FM	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Magic FM	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
TBC International	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Radio Free Africa	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Bongo FM	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Radio Maria	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi

## 2.5 Leseni za huduma za Utangazaji

Mpaka kufikia Machi 2026, kulikuwa na leseni hai 708 kwenye sekta ndogo ya huduma za utangazaji kama inavyooneshwa kwenye jedwali 2.5.1

### Jedwali 2.5.1 Leseni za huduma za Utangazaji

Aina ya leseni	Idadi ya leseni	
	Desemba 2025	Machi 2026
Leseni za Televisheni za Maudhui ya Kitaifa (FTA)	21	21
Leseni za Televisheni za Maudhui ya Wilaya (FTA)	21	21
Leseni za Redio za Maudhui ya Kitaifa	14	14
Leseni za Redio za Maudhui ya Kimkoa	37	37
Leseni za Redio za Maudhui ya Wilaya	188	195
Redio za Jamii	19	20
Televisheni za Maudhui Maalum za Kitaifa	1	1
Televisheni za Maudhui ya Kitaifa za Usajili (Subscription)	30	30
Televisheni za Maudhui ya Wilaya za Usajili (Subscription)	1	1
Utangazaji wa Maudhui ya Kitaifa (Mamlaka ya Kurusha Matangazo) – Wakusanyaji wa Vituo (Wenye Leseni za Miundombinu ya Mtandao na Multiplex)	1	1
Maudhui ya Kitaifa (Huduma Saidizi)	3	3
Wakusanyaji wa Maudhui Mtandaoni	6	6
Blogu	77	74
Redio za Mtandaoni	13	12
Televisheni za Mtandaoni	222	221
Televisheni kwa njia ya waya	55	51

Sura ya tatu 03

# Huduma za Posta na Usafirishaji wa vifurushi na vipeto



# Huduma za Posta na Usafirishaji wa Vifurushi na Vipeto

Sehemu hii inawasilisha muhtasari wa huduma za posta na usafirishaji wa vifurushi nchini Tanzania, ikilenga ushiriki wa wateja na idadi ya vitu kama barua, vifurushi vilivyotumwa na vile vilivyowasilishwa katika mtandao mzima. Katika robo mwaka ulioishia Machi 2026, jumla ya vitu 579,209 vilitumwa na 952,314 vilifikishwa.

## 3.1. Idadi ya masanduku ya posta

Shirika la Posta Tanzania (TPC) linatoa huduma za msingi za posta za masanduku na mifuko binafsi ya barua kwa watu binafsi na kampuni. Idadi ya masanduku na mifuko binafsi katika kipindi cha mwezi Januari hadi Machi 2026, ni kama inavyooneshwa kwenye Jedwali 3.1.1

**Jedwali 3.1.1: Masanduku ya Barua na Mifuko Binafsi ya TPC katika Robo Mwaka Ulioishia Machi 2026**

Mwezi	Masanduku ya barua	Mifuko binafsi ya barua	Jumla
Januari	155,334	67	155,401
Februari	155,334	67	155,401
Machi	155,334	67	155,401

## 3.2. Wateja wa huduma za usafirishaji wa vifurushi na vipeto

Wateja wa huduma za usafirishaji wa vifurushi wamegawanywa katika makundi mawili ambayo ni kampuni na watu binafsi kama inavyooneshwa kwenye jedwali 3.2.1


**Jedwali 3.2.1: Wateja wa huduma za usafirishaji wa vifurushi na vipeto**

	Kampuni/Taasisi	Wateja binafsi	Jumla
Januari	1,016	72,675	73,691
Februari	854	89,290	90,144
Machi	1,010	67,017	68,027

### 3.3. Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa

#### 3.3.1. Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa ndani

Katika robo mwaka ulioishia Machi 2026, idadi ya vitu vilivyotumwa ndani ya nchi ilipungua kwa asilimia 1.4 kutoka vitu 554,261 katika robo mwaka ulioishia Desemba 2025 hadi vitu 546,644 katika robo mwaka ulioishia Machi 2026, kama inavyoonyeshwa katika Kielelezo 3.3.1.1. na Jedwali 3.3.1.1 Kati ya jumla ya vitu vilivyotumwa, TPC ilichangia asilimia 48 (vitu 262,480), huku watoa huduma wengine wa huduma za usafirishaji wa vifurushi wakichangia asilimia 52 (vitu 284,164), kama inavyoonyeshwa katika Kielelezo



Katika kipindi husika, vifurushi vilichangia sehemu kubwa ya vitu vilivyotumwa ndani ya nchi kwa asilimia 39.8, zikifuatiwa na barua (asilimia 29.5), nyaraka (asilimia 21.9), vipeto (asilimia 7.3), na mizigo (asilimia 1.5).


**Jedwali 3.3.1.1: Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa ndani ya nchi kwa robo mwaka iliyoishia Machi 2026**

Mwezi	Barua	Vifurushi	Vipeto	Nyaraka	Mizigo	Jumla
Januari	84,002	76,262	10,917	41,444	1,613	214,238
Februari	44,840	82,665	17,765	39,257	5,383	189,910
Machi	32,580	58,441	11,092	39,189	1,194	142,496
<b>Jumla</b>	<b>161,422</b>	<b>217,368</b>	<b>39,774</b>	<b>119,890</b>	<b>8,190</b>	<b>546,644</b>


**3.3.2. Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi**

Katika robo mwaka ilioishia Machi 2026, idadi ya vitu vilivyotumwa nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 8.3 kutoka vitu 30,065 katika robo mwaka ulioishia Desemba hadi 32,565 katika robo mwaka ulioishia Machi 2026, kama inavyooneshwa katika Kielelezo 3.3.2.1. na Jedwali 3.3.2.1. Aidha, TPC ilichangia sehemu kubwa ya vitu vilivyotumwa kimataifa (vitu 31.189), sawa na asilimia 95.8 ya jumla ya vitu vilivyotumwa, huku watoa huduma wengine wa usafirishaji wa vifurushi wakichangia sehemu ndogo ya vitu 1,376, sawa na asilimia 4.2 ya jumla ya vitu vilivyotumwa. Mgawanyo wa soko kwa vitu vilivyotumwa kimataifa umeoneshwa katika Kielelezo 3.3.2.2.

**Kielelezo 3.3.2.1 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi ('000)**



**Kielelezo 3.3.2.2: Mgawanyo wa bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi baina ya watoa huduma ('000)**



### Jedwali 3.3.2.1: Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi kwa mtoa huduma

Mtoa huduma	Okt - Des 2025	Jan - Mach 2026
TPC	27,877	31,189
Watoa huduma wengine	2,188	1,376
<b>Jumla</b>	<b>30,065</b>	<b>32,565</b>

### Jedwali 3.3.2.2: Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi


Mwezi	Barua	Vifurushi	Vipeto	Nyaraka	Mizigo	Jumla
Januari	9,908	563	77	989	17	11,554
Februari	10,394	207	121	1,118	7	11,847
Machi	8,120	137	30	877	0	9,164
<b>Jumla</b>	<b>28,422</b>	<b>907</b>	<b>228</b>	<b>2,984</b>	<b>24</b>	<b>32,565</b>

## 3.4. Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa

### 3.4.1 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka ndani ya nchi

Katika robo mwaka ulioishia Machi 2026, idadi ya vitu vilivyowasilishwa ndani ya nchi iliongezeka kwa asilimia 11.5 kutoka vitu 814,062 katika robo mwaka ulioishia Desemba hadi 907,759 katika robo mwaka ulioishia Machi 2026. Idadi ya vitu vilivyopokelewa ndani ya nchi imeoneshwa katika kielelezo 3.4.1.1 na Jedwali 3.4.1.1.

**Kielelezo 3.4.1.1 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa ndani ya nchi ('000)**



**Table 3.4.1.1: Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka ndani ya nchi**

Mwezi	Barua	Vifurushi	Vipeto	Nyaraka	Mizigo	Jumla
Januari	183,119	54,779	10,522	40,617	1,426	290,463
Februari	199,412	70,173	16,415	41,026	3,936	330,962
Machi	184,183	50,870	11,125	39,191	965	286,334
<b>Jumla</b>	<b>566,714</b>	<b>175,822</b>	<b>38,062</b>	<b>120,834</b>	<b>6,327</b>	<b>907,759</b>


### 3.4.2. Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi

Katika robo mwaka ulioishia Machi 2026, idadi ya vitu vilivyopokelewa kutoka nje ya nchi ilipungua kwa asilimia 3.9 kutoka vitu 46,362 katika robo mwaka ulioishia Desemba 2025 hadi 44,555 katika robo mwaka ulioishia Machi 2026, kama inavyoonyeshwa katika Jedwali 3.4.2.1. Aidha, TPC ilichangia wingi wa vitu vilivyopokelewa kutoka nje ya nchi (vitu 41,524), ikiwa ni asilimia 93.2 ya jumla ya vitu vilivyopokelewa, huku watoa huduma wengine wa huduma za usafirishaji wa vifurushi wakichangia sehemu ndogo ya vitu 3,031 ikiwa ni asilimia 6.8 ya jumla ya vitu vilivyopokelewa. Mgawanyo wa soko ya vitu vilivyowasilishwa kimataifa imeonyeshwa katika Kielelezo 3.4.2.1. Mgawanyo wa soko kwa vitu vilivyopokelewa kutoka nje ya nchi imeonyeshwa katika Kielelezo 3.4.2.1. Kielelezo 3.4.2.2 na Jedwali 3.4.2.2 yanaonyesha kuwa barua zilichangia sehemu kubwa zaidi ya vitu vilivyotumwa kimataifa katika robo hiyo kwa asilimia 62.4, zikifuatiwa na vipeto (asilimia 22.8), vifurushi (asilimia 8.7) na nyaraka (asilimia 4.2), huku mizigo ya posta ikibaki katika kiwango cha chini sana.


**Jedwali 3.4.2.1: Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi kwa robo mwaka inayoishia Machi 2026**

Watoa huduma	Okt – Des 2025	Jan–Mach 2026
TPC	44,069	41,524
Watoa huduma wengine	2,293	2,946
<b>Jumla</b>	<b>46,362</b>	<b>44,555</b>

**Kielelezo 3.4.2.1 Mgawanyo wa idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi ('000)**



**Kielelezo 3.4.2.2 Mgawanyo wa bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi baina ya watoa huduma ('000)**



**Jedwali 3.4.2.2: Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi katika robo mwaka iliyoishia Machi 2026**

Mwezi	Barua	Vifurushi	Vipeto	Nyaraka	Mizigo	Jumla
Januari	13,507	1,305	4,211	1,144	21	20,188
Februari	7,940	1,455	3,662	515	15	13,587
Machi	7,160	1,108	2,304	208	-	10,780
<b>Jumla</b>	<b>28,607</b>	<b>3,868</b>	<b>10,177</b>	<b>1,867</b>	<b>36</b>	<b>44,555</b>

### 3.5. Ubora wa huduma za Posta na Usafirishaji wa vifurushi na vipeto

Katika kipindi cha robo mwaka kilichoishia Machi 2026, vipimo vya Ubora wa Huduma (QoS) vilifanyika kwa kuzingatia vigezo vya ubora wa huduma (QoS) vilivyoainishwa kwenye Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Ubora wa Huduma), 2025 ili kupima uzingatiaji wa viwango vya muda wa kutuma bidhaa za kiposta.

Katika Kanda A (Inter-Town Zone A), inatakiwa asilimia 90 ya bidhaa za kiposta zipokelewe siku inayofuata (D+1), ambapo asilimia 90 ya watoa huduma wa usafirishaji wa vifurushi na vipeto walikidhi. Kwa upande mwingine, asilimia 74 ya watoa huduma za usafirishaji wa vifurushi na vipeto walikidhi takwa la Kanda B na C kuwa asilimia 90 ya bidhaa za kiposta zinatakiwa zipokelewe ndani ya siku mbili (D+2), kama inavyooneshwa katika Jedwali 3.5.1 na 3.5.2

#### Jedwali 3.5.1: Ubora wa huduma za usafirishaji wa vifurushi na vipeto kanda A (90% ya bidhaa zipokelewe siku inayofuata (D+1))

Mtoa huduma	Hali ya uzingatiaji wa Kanuni
Blaze Concierge And Courier Services Limited	Imekidhi
M/S Azam Marine Company Limited	Imekidhi
H&N Courier Express Limited	Imekidhi
Aifola Express	Imekidhi
Epvate & Fortune International Consulting Limited	Imekidhi
Sga Cash In Transit (T) Limited	Imekidhi
Urban Eagle	Imekidhi
Precision Air Services Plc	Imekidhi
Kapilla Group Limited	Imekidhi
Dorah Ndondi	Imekidhi
Marathon Logistics Limited	Imekidhi
Kimua Company Limited	Imekidhi
Citysprint Fulfilment Center Tanzania Limited	Imekidhi
Geamos Company Limited	Imekidhi
Abc Upper Class & Transportation Limited	Imekidhi
Mwananchi Communications Limited	Imekidhi
Ndengaro Company Limited	Imekidhi
Dhl Tanzania Limited	Imekidhi
Tutume Worldwide Limited	Haijakidhi
Simba Logistic Equipment Supply Co. Ltd	Haijakidhi

**Table 3.5.2: Ubora wa huduma za usafirishaji wa vifurushi na vipeto kanda B na C lengo: Siku +2 (90%)**

Mtoa huduma	Hali ya uzingatiaji wa Kanuni
Geamos Company Limited	Imekidhi
Blaze Concierge And Courier Services Limited	Imekidhi
H&N Courier Express Limited	Imekidhi
Mwananchi Communications Limited	Imekidhi
Aifola Express	Imekidhi
Sga Cash In Transit (T) Limited	Imekidhi
Precision Air Services Plc	Imekidhi
Dorah Ndondi	Imekidhi
Kapilla Group Limited	Imekidhi
Abc Upper Class & Transportation Limited	Imekidhi
Gateway Global Freight Limited	Imekidhi
Kimua Company Limited	Imekidhi
Marathon Logistics Limited	Imekidhi
Citysprint Fulfilment Center Tanzania Limited	Imekidhi
Ndengaro Company Limited	Haijakidhii
Silvus Company Limited	Haijakidhii
Dhl Tanzania Limited	Haijakidhii
Tutume Worldwide Limited	Haijakidhii
Simba Logistic Equipment Supply Co. Ltd	Haijakidhii

TCRA imechukua na itaendelea kuchukua hatua stahiki za kiudhibiti kwa watoa huduma wote walioshindwa kukidhi vigezo vilivyoainishwa kwa mujibu wa kanuni husika.

### 3.6. Leseni za huduma ya posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto

Mpaka kufikia Machi 2026, kulikuwa na leseni hai 144 kwenye sekta ndogo ya huduma za posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto kwenye jedwali 3.6.1

#### Jedwali 3.6.1 Leseni za huduma ya posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto

Aina ya leseni	Idadi ya Leseni	
	Desemba 2025	Machi 2026
Wasafirishaji wa Kimataifa	6	5
Wasafirishaji wa Kati ya Miji	62	56
Wasafirishaji wa ndani ya Jiji	11	8
Wasafirishaji ndani ya Nchi	69	74
Huduma ya Posta kwa Umma	1	1

# Hitimisho

Sekta ya mawasiliano iliendelea kurekodi ukuaji mkubwa katika robo mwaka iliyoishia Machi 2026, ikiakisi mchango wake katika kuendeleza mabadiliko ya kidijiti na maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini. Ongezeko la ueneaji wa miundombinu ya mawasiliano na upatikanaji wa huduma za intaneti ya kasi unachangia kwenye uchumi mpana wa kidijiti nchini kwa kuwezesha ubunifu katika teknolojia ya huduma za kifedha na vifaa vingine vinavyotumia huduma ya intaneti (IoT), kuongeza matumizi ya biashara mtandaoni, na kuimarisha utoaji wa huduma za serikali kidijiti. Hivyo, ukuaji endelevu wa sekta ya mawasiliano hauwezi kutenganishwa na malengo mapana ya Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2050 (TDV-2050).

Katika huduma za mawasiliano ya simu na intaneti, kulikuwa na ongezeko endelevu la usajili, matumizi ya pesa mtandao, na matumizi ya data yanayotokana na kuenea kwa miundombinu ya mtandao wa intaneti ya kasi na kuongezeka kwa matumizi ya vifaa janja. Kumekuwa na ongezeko endelevu la usajili wa laini za simu na matumizi ya data kwa asilimia 4.6 na 15.3, mtawalia. Aidha, matumizi ya huduma za sauti zilipungua kwa asilimia 3.8. Asilimia ya watu waliofikiwa na mtandao wa simu ulifikia 94.32% kwa 4G na 32.83 kwa 5G uliimarisha upatikanaji wa huduma za intaneti ya kasi na kuweka msingi imara wa ushiriki wa nchi katika uchumi wa kidijiti. Usajili wa intaneti uliongezeka kwa asilimia 1.5 na kufikia milioni 58.9 ambayo imechangia kuongezeka kwa idadi ya vikoa vilivyosajiliwa kuongezeka na kufikia 38,409 kwa robo mwaka inayoishia Machi 2026. Huduma za pesa mtandao ziliendelea kukua ambapo idadi ya akaunti za pesa mtandao iliongezeka kwa asilimia 5.9 na hivyo kuimarisha ujumuishwaji wa huduma za kifedha.

Sekta ya utangazaji ilikuwa na mchango katika kusambaza taarifa, kukuza utamaduni na umoja wa kitaifa. Idadi ya watu waliofikiwa na mawimbi ya DTT ilibaki asilimia 58 na FM imefikia asilimia 85.31. Kwa upande mwingine, idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa kifurushi (active decoders) imepungua kwa asilimia 1, na kufikia milioni 2.09 katika kipindi husika.

Huduma za posta na usafirishaji wa vifurushi ziliendelea kubadilika sambamba na ukuaji wa teknolojia na biashara mtandao. TPC iliendelea kuwa kiungo muhimu ikisafirisha bidhaa za kiposta nchini, na kuwaunganisha wananchi na biashara, hususani katika maeneo ya vijijini, kupitia utoaji wa huduma za barua, vifurushi na usafirishaji wa mizigo kwa ufanisi.

Kwa ujumla, matokeo ya robo mwaka inayoishia Machi 2026 yanaonesha kasi endelevu ya ukuaji wa sekta ya mawasiliano kuelekea Tanzania iliyounganishwa zaidi, jumishi na yenye uchumi wa kidijiti. TCRA itaendelea kuweka mazingira wezeshi yanayochochea uwekezaji katika miundombinu, ubunifu, na ukuaji endelevu wa sekta ya mawasiliano kwa mujibu wa vipaumbele vya maendeleo ya taifa na



Mawasiliano Towers,  
20 Sam Nujoma Road,  
14414 Dar es Salaam, Tanzania.  
Barua pepe: dg@tcra.go.tz

 @tcra\_tanzania

